**SURA YA 256**
**SHERIA YA MAPATO YATOKANAYO NA UHALIFU**

**[SHERIA KUU]**

## MPANGILIO WA VIFUNGU

Kifungu Jina


SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA MWANZO

1. Jina fupi
2. Matumizi.
3. Tafsiri.
4. Maana ya “kutiwa hatiani”, n.k., kwa kosa.
5. Maana ya “kukimbia kwa kujificha”
6. Maana ya "kosa kubwa".
7. Maana ya "kujishughulisha na mali".
8. Mahakama inayofaa kuhusiana na kosa kubwa.

SEHEMU YA PILI
UKAMATAJI NA UTAIFISHAJI
Maombi kwa amri ya kutaifisha

9. Ombi kupata amri ya kutaifisha.
10. Notisi ya ombi.
11. Marekebisho ya ombi.
12. Kufanyika kwa amri ya kutaifisha pale mtu ametoroka kwa nia ya kujificha.
13. Utaratibu wa maombi

Amri za kutwaa

14. Amri za kutwaa.
15. Athari ya amri ya kutwaa.
16. Athari ya amri ya kutwaa kwa mtu wa tatu.
17. Kuondoa amri ya kutwaa wakati wa rufaa au wakati wa kutanguliwa hukumu.
18. Usajili wa amri za kutwaa za nje.

SEHEMU YA TATU
AMRI ZA ADHABU ZA KIFEDHA

19. Matumizi ya Sehemu ya III.
20. Masharti maalum kuhusiana na makosa maalum..
21. Amri za adhabu za kifedha.
22. Uhakiki wa adhabu za kifedha.
23. Mahakama inaweza kuinua kinga ya shirika
24. Kiasi kilicholipwa kuhusiana na amri za adhabu za kifedha zilizosajiliwa..

SEHEMU YA NNE
KUTWAA KUHUSIANA NA MAKOSA MAALUM

25. Utwaaji wa mali iliyozuiwa kuhusiana na makosa maalum..
26. Upatikanaji wa mali ambayo kifungu cha 25 kinatumika.

27. Matokeo ya kutangua hukumu.
28. Mtu mwenye manufaa na mali iliyotwaliwa anaweza kununua tena manufaa
29. Kununua manufaa mengine katika mali iliyotwaliwa.
30. Kutwaliwa ambako mtu hawezi kupelekwa mahakamani.

SEHEMU YA TANO
UDHIBITI WA MALI INAYOTAKIWA KUTAIFISHWA
Uwezo wa kupekua na kukamata.

31. Uwezo wa upekuzi na ukamataji mali isiyo safi
31A Kusimamaishwa kwa akaunti.
32. Hati za upekuzi kuhusiana na mali isiyo safi
33. Hati ya upekuzi inaweza kutolewa kwa simu.
34. Upekuzi wakati wa dharura.
35. Uwajibikaji kwa mali iliyokamatwa.
36. kurudishwa kwa mali iliyokamatwa.
37. Upekuzi wa na ukamataji wa mali isiyo safi kuhusiana na makosa yaliyotendeka nje ya nchi.

AMRI ZA KIZUIZI

38. Amri ya kizuizi.
39. Sababu za kutoa amri ya kizuizi.
40. Notisi kwa maombi ya amri ya kizuizi
41. Watu wanaoweza kuwa mbele ya mahakama na kutoa ushahidi.
42. Notisi ya amri ya kizuizi.
43. Mahakama inaweza kutoa amri za ziada
44. Mdhamini kutekeleza amri ya adhabu ya kifedha.
45. Tozo kwa mali kufuatia amri ya kizuizi.
46. Usajili wa amri ya kizuizi
47. Kuvunja amri ya kizuizi.
48. Wajibu wa mdhamini.
49. Kulindwa kwa mdhamini kutoka uwajibikaji binafsi.
50. Ujira na gharama za mdhamini.
51. Mahakama inaweza kufuta amri ya kizuizi
52. Amri ya kizuizi inapokoma kutumika.
53. Amri ya kizuizi ya muda kuhusiana na kosa la nje.
54. Amri ya kizuizi ya nje iliyosajiliwa.
55. Mdhamini kudhibiti mali kuhusiana na amri ya kizuizi ya nje iliyosajiliwa.
56. Shughuli ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
57. Kufutwa kwa amri ya adhabu ya kifedha ya nje.

SEHEMU YA SITA
UWEZO WA KUKUSANYA TAARIFA
Amri za Uwasilishaji

58. Amri za uwasilishaji.
59. Kubadili amri ya uwasilishaji.
60. Kushindwa kutekeleza amri ya uwasilishaji.
61. Amri za uwasilishaji kuhusiana na makosa ya nje.

UWEZO WA UPEKUZI

62. Uwezo wa kupekua hati inayofuatilia mali.

63. Hati ya upekuzi kwa hati inayofuatilia mali.
63A Uchunguzi wa akaunti ya benki
63 B Kuwekwa chini ya ulinzi
63C Ulinzi kwa wachunguzi
63D Ruhusa ya mahakama
64. Hati za upekuzi kuhusiana na makosa ya nje.

AMRI ZA USIMAMIZI

65. Amri za usimamizi.
66. Kutokufichuliwa kwa uwepo wa amri ya usimamizi.
67. Amri za usimamizi kuhusiana na makosa ya nje.

WAJIBU WA TAASISI ZA FEDHA

68. Kimefutwa
69. Kimefutwa
70. Kimefutwa

SEHEMU YA SABA
MASHARTI YA KAWAIDA

71. Fedha haramu.
72. Kukatazwa kujihusisha na mali haramu.
73. Mwenendo wa wakurugenzi, maafisa, waajiriwa au wakala.
74. Kujihusisha na mali iliyotwaliwa.
75. Kigezo cha ushahidi
76. Rufaa.
77. Gharama.
78. Matumizi ya sheria nyingine hautaathirika
79. Kanuni.

**SURA YA 256**
**SHERIA YA MAPATO YATOKANAYO NA UHALIFU**

Sheria ya kuweka masharti bora ya namna ya kushughulikia mapato yatokanayo na uhalifu.

[1 Mei, 1994]
[Gazeti la Serikali Na. 299 ya 1994]
Sheria Na:
25 ya 1991
9 ya 1995

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA MWANZO **(ss 1-8)**

1. Jina fupi

Sheria hii itaitwa Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu.

2. Matumizi

(1) Sheria hii itatumika Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara.

(2) Sheria hii, isipokuwa kifungu cha 57, haitatumika katika kumtia mtu hatiani kwa kosa ikiwa alishatiwa hatiani kwa kosa hilohilo kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

3. Tafsiri Sheria Na 9 ya 1995

(1) Katika Sheria hii, labda kama mazingira yatahitaji vinginevyo:-

"**akaunti**" maana yake ni chombo chochote au utaratibu kupitia taasisi ya fedha inayopokea amana au inayoruhusu utoaji na inajumuisha chombo au utaratibu kwa:-

(a) sanduku la amana ya kudumu ya muda; au
(b) sanduku la usalama la amana ;

**“wakala”** inajumuisha, ikiwa wakala ni kampuni , maafisa na wakala wa hiyo kampuni;

**“afisa anayefaa”** maana yake ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali au mtu katika aina ya watu waliotangazwa na Kanuni kuwa katika maana hii;

**“kuidhinishwa”** maana yake kuidhinishwa na waziri kwa maandishi kwa madhumuni ya masharti ambako usemi huu unatokea.;

**“benki”** maana yake:-

(a) Benki ya Tanzania;
(b) Benki ya watu wa Zanzibar; au
(c) Benki kwa maana iliyopewa chini ya Sheria ya Benki na Taasisi za fedha;

"**manufaa**" inajumuisha huduma au faida;

"**chama cha wajenzi** "maana yake ni chama kilichosajiliwa au au kushirikishwa kama chama cha wajenzi, chama cha ushirika wa nyumba au vyama vinavyofanana chini ya sheria inayotumika kuhusiana na vyama;

"**amri ya kutaifisha**" maana yake ni amri ya kutwaa au amri ya adhabu yenye kuhusika na fedha;

**sheria inayolingana au kufanana "** maana yake ni sheria iliyotangazwa kuwa ni sheria inayofanana au inayolingana na Sheria hii;

"**mkurugenzi**" kuhusiana na taasisi ya fedha na kampuni maana yake ni:-

(a) ikiwa taasisi au kampuni imeanzishwa kwa madhumuni ya umma kwa sheria iliyotungwa na Bunge au Baraza la Mapinduzi, mjumbe wa taasisi au kampuni;

(b) mtu yeyote anayeshikilia au kukaimu nafasi ya mkurugenzi wa taasisi au kampuni kwa jina lolote lile na kama ndio au siyo halali amechaguliwa kushikilia au ameidhinishwa kukaimu katika ile nafasi; na

(c) mtu yeyote kufuatia maelekezo yake wakurugenzi wa taasisi au kampuni wamezoea kuyatekeleza;

**"kizuizi** " kuhusiana na mali, inajumuisha riba, faida, rehani, tozo, haki au dai kuhusiana na mali;

"**afisa mtendaji**" kuhusiana na taasisi ya fedha au kampuni, maana yake ni mtu yeyote, kwa jina lolote lile na kama ndio au siyo mkurugenzi wa taasisi au kampuni, ambaye anahusika, au ana sehemu katika uendeshaji wa taasisi au kampuni;

"**taasisi ya fedha**" maana yake ni-

(a) Benki ya Tanzania;

(b) Benki ya Watu wa Zanzibar;

(c) Chama cha Wajenzi**;**

(d) Taasisi ya fedha kwa maana iliyoko katika Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha;

"**shughuli ya kifedha**" maana yake:–

(a) kufungua, kuendesha, au kufunga akaunti katika taasisi ya fedha;

(b) kufungua au kutumia sanduku la kuweka lililoko katika taasisi ya fedha;

(c) telegrafu au uhamisho kwa elektroni wa fedha na taasisi kwa niaba ya mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine;

(d) upelekaji wa fedha kati ya Jamhuri ya Muungano, nchi za nje au kati ya nchi za nje kwa niaba ya mtu yeyote; au

(e) ombi la mtu yeyote kwa, au upokeaji wa, mkopo kutoka kwa taasisi ya fedha;

"**amri ya kutwaa ya nje**" maana yake amri ya kutwaa chini ya sheria ya nchi za nje na kusajiliwa katika Jamhuri ya Muungano kufuatia kifungu cha 32 cha Sheria ya Kusaidiana *, kwa utekelezaji dhodi ya mali inayosadilkiwa kuwepo katika Jamhuri ya Muungano kuhusiana na kosa kubwa la nje;

"**amri ya adhabu ya kifedha"** maana yake ni amri chini ya sheria ya nchi ya nje na imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano kufuatia kifungu cha 32 cha Sheria ya Kusaidiana *, na ambacho kinatoa adhabu ya fedha kuhusiana na kosa kubwa la nje, lakini haijumuishi amri kwa malipo ya fedha kwa njia ya fidia, urejeshwaji au hasara;

"**amri ya kizuizi ya la nje**" maana yake ni amri chini ya sheria ya nchi ya nje na iliosajiliwa katika Jamhuri ya Muungano kufuatia kifungu cha 32 cha Sheria ya Kusaidiana***** kwa kutekelezwa dhidi ya mali inayosadikiwa kuwepo katika Jamhuri ya Muungano kuhusiana na kosa kubwa la nje;

"**kosa kubwa la nje’’** maana yake ni kosa kubwa lililofanywa kinyume na sheria ya nchi ya nje;

"**amri ya kutwaa**" maana yake ni amri chini ya kifungu cha 14;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama inavyoweza kuwa;

"**riba**" kuhusiana na mali maana yake ni:-

(a) mali halali au ya haki au riba katika mali;au

(b) haki, uwezo au upendeleo kuhusiana na mali, ya sasa au baadaye na kama ipo au isiyotarajiwa**;**

"**wakala wa utekelezaji wa sheria**" maana yake ni jeshi la polisi, na inajumuisha mtu yeyote aliyeruhusiwa kwa maandishi na inspekta jenerali wa polisi kufanya kazi za uchunguzi na ufuatiliaji chini ya Sheria hii;

"**hakimu**" maana yake ni hakimu mkazi;

"**Waziri**" maana yake ni Waziri kwa wakati huu anayeshughulikia masuala ya kisheria;

"**kosa la pesa haramu**" maana yake ni kosa la pesa haramu lililotajwa katika kifungu cha 71;

"**amri ya usimamizi**" maana yake ni amri chini ya kifungu cha 65;

"Sheria ya Kusaidiana" maana yake ni Sheria ya Kusaidiana katika Masuala ya Jinai *;

**"madawa ya kulevya na miharadati"** maana yake ni:–

(a) madawa yaliyokatazwa kufuatia sheria inayotumika kuhusiana na madawa ya kulevya na miharadati;

(b) miharadati iliyotangazwa na sheria yoyote kuwa ni miharadati ambayo tafsiri hii itatumika;

"**afisa**" maana yake ni mkurugenzi, katibu, afisa mtendaji au mfanyakazi;

**"kosa la kawaida linalopelekea kukamatwa"** maana yake ni kosa linalopelekea kukamatwa ambalo si kosa kubwa;

"**kiasi cha adhabu**" kuhusiana na amri ya adhabu ya kifedha dhidi ya mtu, maana yake ni kiasi kile mtu yule anawajibika kulipa chini ya kifungu cha 22;

"**amri ya adhabu ya kifedha**" maana yake ni amri chini ya kifungu cha 22;

"**afisa polisi**" maana yake ni mjumbe yeyote wa kikosi cha polisi wa au juu ya cheo cha koplo;

"**jengo**" itajumuisha:–

(a) umbo, jengo, ndege, gari au chombo;

(b) mahali, kama pamezungushiwa ukuta au kujengwa juu yake au siyo;na

(c) sehemu ya jengo, ikijumuisha jengo la aina iliyotajwa katika aya (a) na (b);

"**mapato"** kuhusiana na kosa, maana yake ni mali yoyote itokanayo, moja kwa moja au si moja kwa moja na mtu yeyote kutokana na utendaji wa kosa;

"**mapato kutokana na kosa" au "faida ya uhalifu**" itatafsiriwa ipasavyo;

"**mapato ya uhalifu**" maana yake ni mali yoyote itokanayo moja kwa moja au si moja kwa moja ,na mtu yeyote kutoka:-

(a) kwenye utendaji wa kosa lolote kubwa;

(b) tendo lolote au kutotenda ambako:-

(i) limetokea nje ya Jamhuri ya Muungano;

(ii) linahusiana na madawa ya kulevya na miharadati; na

(iii) ingekuwa au ikiwa lingetokea katika Jamhuri ya Muungano, ingekuwa ni kosa linalopelekea kukamatwa au kosa kubwa la madawa ya kulevya na miharadati *;na*

"**uzalishaji**" inajumuisha upandaji na utengenezaji;

"**amri ya uwasilishaji** " maana yake ni amri chini ya kifungu cha 62;

"**mali**" maana yake ni mali halisi au mali binafsi ya maelezo yoyote, kama ipo katika jamhuri ya muungano au kwingineko na kama ni dhahiri au si dhahiri na itajumuisha riba katika mali halisi hiyo au mali binafsi;

"**hati ya kufuatilia mali**" maana yake ni hati husika kwa ajili ya:-

(a) kutambua, kuonyesha mahali au kueleza kiasi cha mali ya mtu aliyetenda kosa kubwa;

(b) kutambua au kuonyesha mahali hati yoyote ipo muhimu kwa kuhamisha mali ya mtu aliyetenda kosa kubwa;

(c) kutambua au kuonyesha mahali au kueleza kiasi cha mali haramu kuhusiana na kosa kubwa; au

(d) kutambua au kuonyesha mahali hati yoyote ipo ambayo ni muhimu kwa kuhamisha mali haramu kuhusiana na kosa kubwa;

"**mali isajiliwayo** " maana yake ni mali ambayo umiliki wake unapitishwa kwa usajili katika rejesta iliyowekwa kufuatia masharti ya sheria yoyote;

"**kipindi husika cha maombi** " kuhusiana na kutiwa hatiani kwa mtu kwa kosa linalopelekea kukamatwa, maana yake ni kipindi cha miezi sita baada ya:-

(a) pale mtu atachukuliwa kuwa ametiwa hatiani kwa kosa sababu ya kifungu cha 4(1)(a), siku ile ambayo mtu alitiwa hatiani kwa kosa;

(b) pale mtu atachukuliwa kuwa ametiwa hatiani kwa kosa sababu ya kifungu cha 4(1)(b), siku ile ambayo mtu yule aliachiwa bila hatia;

(c) pale mtu atachukuliwa kuwa ametiwa hatiani kwa kosa sababu ya kifungu cha 4(1)(c ), siku ile mahakama ilipolifikiria katika kupitisha hukumu kwa kosa lile jingine lililotajwa katika aya (c); au

(d) pale mtu atachukuliwa kuwa alitiwa hatiani sababu ya kifungu cha 4 (1)(c), siku ile ambayo mtu yule itachukuliwa kuwa alikimbia kwa kujificha kuhusiana na kosa;

"**kosa husika**", kuhusiana na mali haramu, maana yake ni kosa kwa sababu ya utendaji ambao mali ni mali haramu;

"**amri ya zuio**" maana yake ni amri chini ya kifungu cha 38;

"**kosa kubwa la madawa ya kulevya na miharadati**" maana yake ni kosa lolote linalohusiana na madawa ya kulewa na miharadati:-

(a) ambalo linaadhibiwa katika Jamhuri ya Muungano au katika nchi ya nje kwa kifungo cha kipindi kisichopungua miaka mitatu au kwa kwa adhabu kali zaidi; au

(b) bei ya soko ya mali iliyotokana au iliyopatikana kutoka katika utendaji ambao ni au unaoweza kuwa si chini ya shilingi milioni mbili au kiasi kikubwa zaidi au kidogo zaidi kama itakavyoweza kuagizwa;

"**kosa kubwa** " maana yake ni kosa lolote lilioagizwa hivyo na au chini ya kifungu cha 6 na itajumuisha kosa maalum;

"**kosa maalum** " maana yake ni:–

(a) kosa kubwa la madawa ya kulevya na miharadati**;**

(b) pesa haramu kinyume na kifungu cha 71;

(c) kosa lingine lolote ambalo Waziri anaweza kwa amri iliyochapishwa katika *Gazeti la Serikali*, kuagiza hivyo, kufuatia idhini ya Azimio la Bunge;

(d) kula njama ya kufanya, au kusaidia, au kusaidia katika jinai, kushauri au kusaidia utendaji wa kosa lililotajwa katika aya za (a), (b) au (c);

(e) kumsaidia mtu mwingine kutumia mapato yatokanayo na kosa chini ya aya ya (a); au

(f) kujaribu kutenda kosa chini ya aya za (a), (b) au (c);

**"mali haramu",** kuhusiana na kosa kubwa, maana yake ni:-

(a) mali yoyote inayotumika katika, au kuhusiana na utendaji wa hilo kosa; au

(b) mali yoyote katika Jamhuri ya Muungano ambayo ni pato litokanalo na kosa kubwa la nje kuhusiana na amri inayoweza kusajiliwa chini ya Sehemu ya Nne ya Sheria ya Kusaidiana na ikitumika bila kurejea katika kosa fulani maana yake ni mali haramu kuhusiana na kosa linalopelekea kukamatwa**;**

"**mdhamini** " maana yake ni muamana aliyechaguliwa na Mahakama Kuu chini ya aya (b) ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 38;

"**shughuli isiyo halali**" maana yake ni kitendo au kutotenda ambako ni kosa chini ya sheria yoyote inayotumika kwa wakati huu katika Jamhuri ya Muungano.

(2) Rejeo katika sheria hii kwa mtu ambaye ameshtakiwa kwa kosa ni rejeo kwa taarifa iliyowekwa dhidi ya mtu kwa kosa ikiwa kama au siyo:-

(a) hati ya kuhitaji mahudhurio ya mtu kujibu taarifa iliyokwisha kutolewa; au

(b) hati ya kumkamata mtu iliyokwisha kutolewa.

(3) Rejeo katika Sheria hii kwa manufaa yapatikanayo, moja kwa moja au si dhahiri, na mtu mwingine, kwa mtu kwa ombi au maelekezo ya mtu wa kwanza.

(4) Rejeo lolote katika Sheria hii kwa mali ya mtu itajumuisha rejeo kwa mali kuhusiana na mtu mwenye manufaa nayo.

(5) Rejeo katika Sheria hii la kupata mali au manufaa katika mali, kwa malipo yanayotosheleza ni rejeo la kumpatia mali au manufaa kwa malipo yanayotosheleza na kwamba, ukiangalia malipo ya kibiashara tu, inaonyesha thamani ya mali au ya manufaa.

(6) Kwa madhumuni ya Sheria hii, mtu hatachukuliwa kuwa ni mkurugenzi kwa maana ya aya (c ) ya tafsiri ya "mkurugenzi"katika kifungu kidogo cha (1) kwa sababu tu mkurugenzi anatekeleza kwa ushauri anaopewa naye katika utekelezaji bora wa kazi zinazoambatana na uwezo wake wa kitaaluma au uhusiano wa biashara na wakurugenzi wa taasisi ya fedha au kampuni,kama inavyoweza kuwa.

4. Maana ya **"kutiwa hatiani",** n.k., ya kosa ni:-

(1) Kwa madhumuni ya Sheria hii mtu atachukuliwa kuwa ametiwa hatiani kwa kosa ikiwa:-

(a) ametiwa hatiani, ametiwa hatiani, ama bila haki ya kujitetea au vinginevyo, kwa kosa;

(b) ameshitakiwa kwa, na amekutwa ana kosa na kuhukumiwa kwa kosa lakini akaachiwa kwa masharti au bila ya masharti au akasamehewa;au

(c) mtu amekimbia kwa kujificha kuhusiana na kosa hilo.

(2) Kifungu hiki hakitatumika kwa kosa kubwa la nje.

5. Maana ya **"kukimbia kwa kujificha"**

Kwa madhumuni ya Sheria hii, isipokuwa kifungu cha 4,mtu atachukuliwa kuwa amekimbia kwa kujificha kuhusiana na kosa ikiwa na ikiwa tu:-

(a) taarifa imewekwa ikidai utendaji wa kosa na mtu yeyote;

(b) hati ya kumkamata mtu imetolewa kuhusiana na taarifa iliyotolewa;na (c) kimojawapo kati ya hivyo kutokea,ambavyo ni:-

(i) mtu amefariki kabla ya hati kutekelezwa;

(ii) mwishoni mwa kipindi cha miezi sita kutoka kwa tarehe ya kutolewa kwa hati:-

(aa) mtu yule imeshindikana kupatikana; au

(bb) mtu yule, kwa sababu ingine yoyote, si mtiifu wa sheria na ikiwa mtu yule yuko nje ya Jamhuri ya Muungano, mashtaka ya urejeshwaji hayajaanzishwa;

(iii) mwishoni mwa kipindi cha miezi sita kutoka siku ya kutolewa hati:-

(aa) mtu yule kwa sababu ya kuwa nje ya Jamhurui ya Muungano, si mtiifu wa sheria**;**

(bb) mashtaka ya urejeshwaji yameanzwa, na mashtaka hayo yamesimama bila ya amri kwa ajili ya urejeshwaji wa mtu huyo kufanywa.

6. Maana ya **"kosa kubwa"** katika sheria hii, msemo "kosa kubwa" maana yake ni:–

(a) shughuli yoyote ambayo ni sawa na usafirishaji wa madawa ya kulevya chini ya sheria inayotumika kuhusiana na madawa;

(b) kosa lolote bayana;

(c) kosa lolote ambalo Waziri anaweza, kwa amri kuchapisha katika Gazeti la Serikali, lililoagizwa kufanya hivyo, kufuatia idhini kwa Azimio la Bunge.

7. Maana ya **"kujishughulisha na mali"** Kwa madhumuni ya Sheria hii, kujishughulisha na mali ya mtu inajumuisha:-

(a) kama ni deni analodaiwa mtu huyo, kufanya malipo kwa mtu yeyote kwa kupunguza kiasi cha deni;

(b) kutoa mali kutoka Jamhuri ya Muungano;

(c) kupokea au kutoa zawadi ya mali.

8. Mahakama inayofaa kuhusiana na kosa Kubwa;

Pale mtu ametiwa hatiani kwa kosa kubwa mbele ya mahakama yoyote zaidi ya mahakama ya mwanzo mahakama ile itakuwa ni mahakama inayofaa kuhusiana na hukumu hiyo.

## SEHEMU YA PILI
## UKAMATAJI NA UTAIFISHAJI (vif. 9-18)
### Ombi kupata amri ya kutaifisha (vif. 9-13)

Ombi kupata amri ya utaifishaji

9. - (1) Pale mtu ametiwa hatiani kwa kosa kubwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza, kufuatia kifungu kidogo cha (2), kuomba kwa mahakama iliyotoa hukumu au kwa mahakama nyingine yoyote inayofaa, si chini ya miezi sita baada ya kutiwa hatiani mtu yule, kwa:-

(a) amri ya kutwaa dhidi ya mali yoyote ambayo ni haramu kuhusiana na kosa; au

(b) amri ya adhabu yenye kuhusika na fedha dhidi ya mtu kuhusiana na manufaa yatokanayo na mtu kutoka katika utendaji wa kosa;

(2) Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa ruhusa ya mahakama hatapeleka ombi chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa amri ya kutwaa au amri ya adhabu yenye kuhusika na fedha:-

(a) ikiwa ombi lilikwisha kupelekwa chini ya kifungu kidogo hicho au chini ya sheria nyingine yoyote; na

(b) ombi limekwishatolewa uamuzi kuhusu ustahili wake.

(3) Mahakama haitatoa ruhusa chini ya kifungu kidogo cha (2) mpaka ijiridhishe kwamba:-

(a) mali haramu, au manufaa yanayotokana na ombi jipya linalohusiana lilitambuliwa tu baada ya ombi la mwanzo kuamuliwa;

(b) ushahidi wa lazima ulipatikana tu baaday a ombi la mwanzo kuamuliwa; kwa manufaa ya haki kutoa ruhusa.

(4) Ombi linaweza kupelekwa chini ya kifungu hiki kuhusiana na kosa moja au zaidi linalopelekea kukamatwa**.**

(5) Ombi linaweza kupelelkwa chini ya kifungu hiki kwa amri ya adhabu ya kifedha kuhusiana na kosa hata kama kifungu cha 26 kinatumika kwa kosa hilo.

Notisi ya ombi

**10.**-(1) Pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali amepeleka ombi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 9 kwa amri ya kutwaa dhidi ya mali kuhusiana na mtu kuhukumiwa kwa kosa:–

(a) Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatoa notisi ya ombi hilo kwa mtu au mtu mwingine yeyote atakayekuwa na sababu za kuamini anaweza kuwa na manufaa na mali hiyo;

(b) mtu yule, na mtu mwingine yeyote anayedai kuwa na manufaa katika mali hiyo, anaweza kutokea na kutoa ushahidi katika kusikilizwa kwa ombi hilo;na

(c) mahakama inaweza, wakati wowote kabla ya uamuzi wa mwisho wa ombi kwa mtu maalum au aina ya watu kwa namna na kwa wakati ule ambao mahakama inaona kufaa.

(2) Pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali anapeleka ombi kwa amri ya adhabu ya kifedha dhidi ya mtu:–

(a) Mwanasheria Mkuu wa Serikali atampa mtu yule notisi ya maandishi ya ombi hilo;na

(b) mtu yule anaweza kutokea na kutoa ushahidi wakati wa kusikilizwa kwa ombi hilo.

Marekebisho ya ombi

**11.** - (1) Kufuatia kifungu kidogo cha (2), pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali anapeleka ombi kupatiwa amri ya utaifishaji, mahakama inaposikiliza ombi hilo inaweza kubadili ombi kwa kuombwa au kwa ruhusa,ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(2) Mahakama inaweza isibadili ombi ili kuhusisha mali ya ziada katika ombi la kupatiwa amri ya kutwaa au manufaa ya ziada katika ombi la kupatiwa amri yenye adhabu ya kifedha mpaka ikijiridhisha kwamba:-

(a) ile mali au manufaa haikuwa na uwezekano unaoweza kutambuliwa pale ombi la mwanzo lilipofanywa; au

(b) ushahidi wa lazima ulipatikana pale tu ombi la mwanzo lilipofanywa. (3) Pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali anapoomba mabadiliko ya ombi la kupatiwa amri ya kutwaa na badiliko limekuwa na au lingeweza kuwa na matokeo ya kuhusisha mali ya ziada katika ombi la amri ya kutwaa; ndipo-

(a) Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatoa notisi ya maandishi ya kuomba kufanya mabadiliko kwa mtu yeyote ambae ana sababu za kuamini anaweza kuwa na manufaa katika mali kuhusishwa katika ombi la kupatiwa amri ya kutwaa;

(b) mtu yeyote anayedai kuwa na manufaa katika mali itakayojumuishwa katika ombi la amri ya kutwaa anaweza kutokea na kutoa ushahidi katika kikao cha kusikiliza ombi la mabadiliko.

(4) Pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali ataomba badiliko la ombi kwa amri ya adhabu ya kifedha dhidi ya mtu na badiliko lina au lingeweza kuwa na matokeo ya kujumuisha manufaa ya ziada katika ombi kwa amri yenye adhabu ya kifedha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atampa mtu yule notisi ya maandishi ya ombi la badiliko.

Kufanyika kwa amri ya utaifishaji pale mtu ametoroka kwa nia ya kujificha.

**12.** Pale mtu, kwa sababu ya kifungu cha 4(1) (c), amechukuliwa kuwa ametiwa hatiani kwa kosa linalopelekea kukamatwa, mahakama haitatoa amri ya utaifishaji ikitegemea hukumu ya mtu yule kwa lile kosa mpaka mahakama ijiridhishe, kwa dhana ya uwezekano wa kutenda ama kutotenda kosa, kwamba yule mtu ametoroka kwa nia ya kujificha na-

(a) mtu yule amekabidhiwa mahakamani kushitakiwa kwa kosa; au

(b) mahakama ikiridhika kwamba ikizingatia ushahidi wote uliotolewa, mahakama adili inaweza kwa haki kisheria kumwona mtu kuwa ametenda kosa.

Utaratibu wa maombi

**13.** - (1) Pale ombi linapelekwa mahakamani kwa amri ya kutaifisha kuhusiana na hukumu ya mtu kwa kosa kubwa,mahakama inaweza,katika kuamua kuhusu ombi hilo itazingatia kumbukumbu ya mwenendo dhidi ya mtu yule kuhusiana na kosa.

(2) Pale ombi linapelekwa kwa amri ya kutaifisha mahakama ile iliyomhukumu mtu huyo na mahakama hiyo haijapitisha hukumu wakati ombi linafanywa,mahakama inaweza,ikiridhika kwamba ni adili katika mazingira hayo kuacha kupitisha hukumu mpaka ipitie na kuamua ombi la amri ya kutaifisha**.**

(3) Pale itakapochukuliwa kuwa mtu amehukumiwa kwa kosa kwa sababu ya kifungu cha 4(1)(c ),ombi limepelekwa mahakamani kwa amri ya kutaifisha kuhusiana na hukumu,marejeo kwa kifungu kidogo cha (1) kwa mwenendo dhidi ya mtu kwa kosa a lingine lililorejewa katika aya hiyo.

Amri za kutwaa

**14. -** (1) Pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali anapopeleka ombi mahakamani kwa amri ya kutwaa chini ya kifungu cha 9 dhidi ya mali ya mtu aliyehukumiwa kwa kosa na mahakama ikiridhika kwamba mali ni mali haramu kuhusiana na kosa,mahakama ikiona inafaa itaamuru mali hiyo au mali iliyotajwa katika amri hiyo, itwaliwe na Jamhuri ya Muungano..

(2) Pale mahakama itaamuru kwamba mali ambayo si fedha itwaliwe na Jamhuri ya Muungano, lazima iseme bayana katika amri hiyo kiasi kile inachoona ni thamani ya mali kwa wakati ule amri inapotolewa.

(3) Katika utoaji wa ombi la amri ya kutwaa kuhusiana na mali yoyote, mahakama inaweza kuzingatia yafuatayo-

(a)ugumu wowote unaoweza kutegemewa kusababishwa kwa mtu yeyote kutokana na utekelezaji wa amri hii;

(b) utumiaji wa kawaida uliofanywa,au uliopangwa kufanywa wa mali hiyo; (c) ukubwa wa kosa husika.

(4) Ushahidi wowote uliotolewa wakati wa kusikilizwa kwa ombi kw ajili ya amri ya kutwaa kuhusiana na mali yoyote kwamba mali husika ilikuwa chini ya umiliki wa mtu aliyehukumiwa wakati ule, au mara baada, ya utendaji wa kosa na hakuna ushahidi uliotolewa kuonyesha kwamba mali haikutumika katika au kuhusiana na utendaji wa kosa, mahakama itachukulia kwamba mali ilitumika katika, au kuhusiana na utendaji wa kosa.

(5) katika utoaji wa ombi kwa amri ya kutwaa,mahakama inaweza kutoa maelekezo yoyote muhimu au muafaka ili kufanya amri itekelezeke,ikiwa ni pamoja na ,bila kuathiri ujumla wa masharti yaliyotangulia,maelekezo kwa afisa wa mahakama kufanya chochote muhimu na adili ili kupata umiliki wa waraka wowote muhimu kwa kuhamisha mali yoyote kufuatia usajili katika ofisi ya Msajili wa Hati.

(6) Katika utoaji wa amri ya kutwaa mahakama inaweza,ikiridhika kwamba itakuwa kwa manufaa ya umma,manufaa ya mtu katika mali ile kuhamishiwa kwake,iamue asili,kiwango na thamani ya manufaa na itangaze kwamba amri ya kutwaa inaweza,kwa kiwango kile kinachohusiana na manufaa,iachiliwe kufuatana na kifungu cha 30.

Athari ya amri ya kutwaa

**15. -** (1)Kufuatia kifungu kidogo cha (2), pale mahakama imetoa amri ya kutwaa dhidi ya mali, mali ile itapewa Jamhuri ya Muungano

(2) Pale amri ya kutwaa imetolewa dhidi ya mali kufuatia usajili katika ofisi ya Msajili wa Hati haki zozote katika mali zitakuwa za Jamhuri ya Muungano mpaka usajili utakapokamilika

(3)Msajili wa Hazina atasajiliwa kama mmiliki wa mali yoyote kufuatia amri ya kutwaa na waziri atafanya au ataamuru kitu chochote muhimu au muafaka kifanyike kupata usajili wa Msajili wa Hazina kama mmiliki,ikihusisha utekelezaji wa hati rasmi inayotakiwa kutekelezwa na mtu anayehamisha manufaa katika mali ya asili hiyo.

Athari ya amri ya kutwaa kwa mtu wa tatu

**16. -** (1) Pale ombi la amri ya kutwaa inafanywa dhidi ya mali, mtu yeyote mwenye manufaa katika mali anaweza, kabla ya amri ya kutwaa haijatolewa kutuma ombi mahakamani chini ya kifungu kidogo cha (6 (2) kufuatia kifungu kidogo cha (6) na(7) ,pale amri ya kutwaa dhidi ya mali imefanywa mtu yeyote mwenye manufaa katika mali ile anaweza kutuma ombi mahakamani kupata amri chini ya kifungu kidogo cha (6)

(3) Mtu aliyetoa notisi ya ombi la amri ya kutwaa au aliyekuwepo kwenye kusikilizwa kwa ombi hatapeleka ombi mahakamani kufuatia kifungu kidogo cha (2) bila ya ruhusa ya mahakama.

(4) Ruhusa ya mahakama iliyorejewa katika kifungu kidogo cha (3) inaweza kutolewa iwapo mahakama itaridhika kwamba kuna sababu maalum za kutoa ruhusa hiyo.

(5) Bila kuathiri masharti ya ujumla ya kifungu kidogo cha (4), mahakama inaweza kumpatia mtu ruhusa kupeleka mombi kama ikiridhika kwamba ushahidi ambao mtu yule alikusudia kutoa kuhusiana na ombi chini ya kifungu kidogo cha (2) hakuwa nao wakati wa kusikilizwa kwa ombi hilo

(6) Pale mtu anatuma ombi mahakamani kupata amri chini ya hiki kifungu kidogo kuhusiana na manufaa katika mali dhidi ya ombi la kupatiwa amri ya kutwaa au amri ya kutwaa imetolewa na mahakama imeridhika kwamba-

(a) mtuma ombi hakuwa kwa namna yoyote kuhusika na utendaji wa kosa husika;au

(b) iwapo mtuma ombi amepata manufaa yake kwa wakati ule au baada ya utendaji wa kosa,mtuma ombi alifanya hivyo:-

(i) kwa thamani ya kutosha; na

(ii) bila kujua na katika mazingira ambayo hayasababishi wasiwasi ulio makini kwamba mali ile ilikuwa wakati imepatikana, mali haramu, mahakama itaamuru kwa amri uhamishaji wa manufaa na Msajili wa Hazina kwa mtuma ombi ya kiasi kilicho sawa na thamani ya manufaa, kama mahakama itakavyoona inafaa **.**

(7) Kufuatia kifungu kidogo cha (8), ombi chini ya kifungu kidogo cha (2) litapelekwa kabla ya kuisha kwa kipindi cha miezi sita kuanzia siku ile amri ya kutwaa ilipotolewa**.**

(8) Pale amri ya kutwaa inakuwa imetolewa dhidi ya mali, mahakama iliyotoa amri hiyo inaweza,kwa ombi lililopelekwa kwake,kumpatia mtu anayedai manufaa katika mali ruhusa kutuma ombi chini ya kifungu kidogo cha (2),baada ya kumalizika kwa kipindi kilichorejewa chini ya kifungu kidogo cha (7) iwapo itaridhika kwamba kushindwa kwa mtu yule kutuma maombi katika kipindi hicho haikuwa kwa uzembe kwa upande wake.

(9) Mtu yeyote anayetuma maombi kufuatia kifungu cha (1) au cha (2) atamjulisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali**.**

(10) Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa mhusika katika kesi akituma maombi kufuatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) au cha (2).

Kuondoa amri ya kutwaa kwa rufaa au kutanguliwa kwa hukumu

**17. -** (1) Amri ya kutwaa dhidi ya mali itaondolewa kufuatia kufutwa kwa hukumu ambayo amri ya kutwaa ilihusika.

(2) Pale amri ya kutwaa dhidi ya mali imeondolewa kufuatia kifungu kidogo cha (1) au kwa rufaa dhidi ya kufanyika kwa amri hiyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali:**–**

(a)haraka iwezekanavyo baada ya kuondolewa kwa amri hiyo, atatoa notisi ya maandishi ya kuondoa amri kwa mtu yeyote ambaye anaamini ana manufaa katika mali hiyo mara kabla ya kufanyika kwa amri hiyo;au

(b)akihitajika na mahakama kuchapisha katika *Gazeti la Serikali*, notisi ya kuondolewa kwa amri kwa namna na katika kipindi kama mahakama itakavyoona inafaa.

(3) Notisi iliyorejewa katika kifungu kidogo cha (2) itaweka bayana, kufuatia kifungu kidogo cha (4), kwa namna ambayo mtu yeyote anayedai kuwa na manufaa katika mali anaweza kutuma maombi ya kuhamisha manufaa kwa mtu yule**.**

(4) Pale amri ya kutwaa inaondolewa kufuatia kifungu kidogo cha (1) au kwa rufaa dhidi ya kutolewa kwa amri hiyo,mtu yeyote ambae mara baada ya kutolewa kwa amri hiyo,anadai kuwa na manufaa katika mali anaweza kutuma ombi kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maandishi,kwa uhamisho wa manufaa kuja kwake na Mwanasheria Mkuu wa Serikali akipokea **-**

(a) pale manufaa yapo kwa Msajili wa Hazina, ataandaa uhamisho wa manufaa kwa mtu huyo; au

(b) katika suala lingine lolote, atamlipa mtu huyo kiasi cha fedha kinacholingana na thamani ya manufaa hayo.

(5) Pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali anapotakiwa kuandaa uhamisho wa mali kwa mtu, anaweza kufanya hivyo au kuamuru lifanywe jambo lolote muhimu au muafaka ili kuhamisha, ikijumuisha na utekelezaji wa hati rasmi yoyote na kutolewa kwa ombi la usajili wa manufaa katika mali hiyo**.**

Usajili wa amri za kutwaa za nje

**18. -** (1)Pale amri ya kutwaa ya nje imesajiliwa Mahakama Kuu kufuatana na Sehemu ya Nne ya Sheria ya Kusaidiana, Sehemu hii itatumika vivyo hivyo kwa amri yoyote ya nje (2) mali yoyote inayohusiana na amri ya kutwaa ya nje iliyosajiliwa kufuatana na kifungu kidogo cha (1) inaweza kumalizwa au kushughulikiwa vinginevyo kufuatana na maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali au ya mtu aliyepewa mamlaka hayo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maandishi kwa madhumuni hayo**.**

## SEHEMU YA TATU
## AMRI YA ADHABU YA KIFEDHA

Matumizi ya Sehemu ya Tatu

**19. -** Sehemu hii itatumika kwa:**–**

(a) mali ambayo imekuja katika umiliki au usimamizi wa mtu, akiwa ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano na kama kabla au baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii; na

(b) manufaa yaliyomfikia mtu, akiwa ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano na kama kabla au baada ya kuanza kutumika kwa sheria hii.

Masharti maalum kuhusiana na makosa maalum.

**20.** Ombi la amri ya adhabu ya kifedha dhidi ya mtu kuhusiana na hukumu yake kwa kosa maalum haitatolewa na mahakama kabla ya kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe ile ya hukumu iliyohusiana na ombi au baada ya kipindi cha miezi kumi na mbili toka tarehe ya ile hukumu.

Amri ya adhabu ya kifedha

**21.** - (1) Pale ambapo ombi litakapopelekwa mahakamani kwa amri ya adhabu ya kifedha kuhusiana na manufaa anayopata mtu kutokana na utendaji wa kosa na mahakama ikiridhika kwamba mtu yule alipata manufaa kutokana na utendaji wa kosa hilo, mahakama inaweza, kufuatia masharti ya kifungu cha 22, kutathmini thamani ya manufaa yaliyopatikana kumwamuru mtu huyo kumlipa Msajili wa Hazina kufuatana na kifungu cha (2) na cha (3), adhabu ya kifedha iliyo sawa na thamani ya manufaa yaliyokadiriwa.

(2) Pale ambapo mali inayotokana na uhalifu imetwaliwa kufuatana na masharti ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote au kwa amri ya kutwaa inapendekezwa kutolewa dhidi ya mali ambayo imetokana na uhalifu, adhabu

iliyorejewa katika kifungu kidogo cha (1) itapunguzwa kwa kiasi kinacholingana na thamani wakati wa kutolewa kwa amri ya adhabu ya kifedha ya mali iliyotwaliwa.

(3) Iwapo kiasi cha kodi, kwa vyovyote vile iwe chini ya sheria za Tanzania au ya nchi ya nje, imelipwa na mtu na kwamba kodi inahusika yote au kwa sehemu na manufaa kuhusiana na amri ya adhabu ya kifedha inayotolewa, kiasi kile kinaweza, iwapo mahakama itaelekeza hivyo, kupunguzwa kutoka kwenye adhabu iliyothaminiwa kufuatia masharti ya kifungu kidogo cha (1).

(4) Mahakama inaweza kupunguza kiasi kilicholipwa na mtu chini ya amri ya adhabu ya kifedha iliyotolewa kuhusiana na kosa kwa kiasi kinacholingana na kiasi kilicholipwa na mtu kwa njia ya kurudisha upya, kufidia, uharibifu au faini kuhusiana na kosa.

(5) Katika kupiga hesabu ya kiasi kinacholipwa chini ya amri ya adhabu ya kifedha, iwapo mahakama ilizingatia utwaaji wa,au amri ya adhabu ya kutwaa iliyopendekezwa kuhusiana na mali na rufaa dhidi ya amri ya kutwaa inaruhusiwa au kesi ya amri ya kutwaa iliyopendekezwa itasimamishwa kabla ya amri kutolewa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kuomba mahakama kubadilisha amri ya adhabu ya kifedha kwa kuongeza thamani ya adhabu kwa thamani ya mali husika na mahakama inaweza kubadili amri hiyo ipasavyo.

(6) Katika kupiga hesabu ya kiasi kitakacholipwa chini ya amri ya adhabu ya kifedha, iwapo mahakama ilizingatia kiasi cha kodi kilicholipwa na mtu yule na kiasi kimelipwa tena au kurudishwa kwa mtu kuhusiana na kodi iliyolipwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kuomba mahakamani ili kubadili amri ya adhabu ya kifedha ili kuongeza adhabu ya kifedha kwa kiasi kile kilicholipwa tena au kurudishwa na mahakama inaweza kubadili amri hiyo ipasavyo.

(7) Kiasi chochote kinacholipwa na mtu kwenda kwa Jamhuri ya Muungano kufuatia masharti ya amri ya adhabu ya kifedha itakuwa ni deni kwa njia ya kesi ya madai kwa Jamhuri ya Muungano na zitapatikana kwa utaratibu wa mwenendo wa madai.

Mhakiki wa adhabu ya kifedha

22. - (1) Kwa madhumuni ya amri adhabu ya kifedha dhidi ya mtu (ambaye hapa atajulikana kama (‘’mlalamikiwa”) thamani ya manufaa aliyopata mlalamikiwa kutokana n a utendaji wa kosa itakadiriwa na mahakama ikizingatia:–

(a) kiasi cha fedha au thamani ya mali iliyokuja kwenye umiliki au usimamizi wa:-
  (i) mlalamikiwa; au
  (ii) mtu mwingine yeyote kwa ombi au maelekezo ya mlalamikiwa, katika kutenda wa kosa;
(b) thamani ya manufaa mengine yoyote aliyoyapata:-
  (i) mlalamikiwa; au
  (ii) mtu mwingine yeyote kwa ombi au maelekezo ya mlalamikiwa katika kutenda kosa;
(c) iwapo kosa linahusika na kufanya jambo au kitu kuhusiana na madawa ya kulevya na miharadati:-
  (i) bei ya soko, wakati wa utendaji wa kosa, linalofanana au kukaribia kufanana na madawa ya kulevya na miharadati; na
  (ii) kiasi kile kilichokuwa, au kwa kadri au kiasi kile kilichokuwa kilipwe kwa kufanya kitu kinachofanana au kitendo au kitu kukaribia kufanana;
(d) thamani ya mali ya mlalamikiwa kabla na baada ya utendaji wa kosa; na
(e) kipato cha mlalamikiwa na matumizi yake kabla na baada ya kosa.

(2) Katika kukadiria thamani ya manufaa kwa madhumuni ya kifungu hiki mahakama inaweza kuifanya thamaniya manufaa kuwa thamani ile ambayo ingekuwa

kama manufaa hayo yangepatikana wakati uthatmini unafanywa na inaweza kuzingatia kushuka kwa uwezo wa kununua wa kifedha kati ya wakati manufaa yalipatikana na wakati utathmini ulifanywa.

(3) Pale ambapo ombi linafanywa kwa amri ya adhabu ya kifedha dhidi ya mali ya mtu kuhusiana na kosa kubwa na sio kosa maalum:-

(a) iwapo ushahidi uliotolewa kwamba thamani ya mali ya mtu baada ya utendaji wa kosa umezidi kabla ya utendaji wa kosa, mahakama kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 23 kwa kuzingatia aya ya (b) na kifungu kidogo cha (7), kuifanya thamani ya manufaa inayopatikana na mtu kwa utendaji wa kosa kuwa si chini ya kiasi kile kilichozidi;

(b) iwapo, kufuatia ushahidi uliorejewa chini ya aya ya (a),mtu yule atairidhisha mahakama kwamba:-

(i) kiasi chote cha kiasi kichozidi kufuatia sababu zisizohusiana na utendaji wa kosa, aya ya (a ) haitatumika;au

(ii) sehemu ya kiasi kilichozidi kimesababishwa na sababu zisizohusiana na utendaji wa kosa, aya ya (a) haitatumika tu kwa ile sehemu ya kiasi kilichozidi ambacho kinahusiana na utendaji wa kosa.

(4) Pale ombi limetolewa kwa amri ya adhabu ya kifedha dhidi ya mali ya mtu kuhusiana na kosa au makosa maalum:–

(a) mali yote ya mtu huyo wakati ombi linafanywa; na

(b) mali yote ya mtu yule wakati wowote ule:-

(i) kati ya siku ya kosa, au kosa la mwanzo liliolofanywa na siku ambayo ombi lilifanywa; au

(ii) kati ya kipindi cha miaka mitano mara tu baada ya siku ambayo ombi lilifanywa,

itakuwa kile ambacho ni kifupi,itachukuliwa labda kama kinyume chake itathibitishwa kuwa ni mali iliyokuja kwenye umiliki au chini ya usimamizi wa mtu kwa sababu za utendaji wa kosa au makosa maalum.

(5) Faida isizingatiwe kwa madhumuni ya kifungu hiki iwapo adhabu ya kifedha imetolewa kuhusiana na faida hiyo kufuatia masharti chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, pale ambapo mali ya mtu imewekwa chini ya udhamini wa ufilisi wa mtu, mali hiyo itachukuliwa kuendelea kuwa mali ya mtu yule.

(7) Wakati wa kusikiliza ombi kwa ajili ya amri ya adhabu ya kifedha, afisa polisi ambaye ana uzoefu katika uchunguzi wa makosa ya madawa ya kulevya na miharadati anaweza kutoa ushahidi, kwa kadri ya taarifa ,ujuzi na imani yake:–

(a) kuhusu thamani ya soko ya madawa ya kulevya na miharadati kwa wakati fulani au kwa kipindi fulani;

(b) kuhusu bei au kadiri ya bei zinazolipwa kwa kipindi fulani kwa kutenda jambo au kitu kinachohusiana na madawa ya kulevya na miharadati,

bila ya kujali sheria yoyote au utendaji wowote unaohusiana na ushahidi wa kusikia ,na ushahidi wa haswa wa masuala yanayotolewa ushahidi.

Mahakama inaweza kunyanyua kinga ya shirika

**23. -** (1) Katika kukadiria thamani ya faida aliyopata mtu kwa utendaji wa kosa kubwa, mahakama inaweza kuifanya kama mali ya mtu mali yoyote ambayo katika mawazo ya mahakama ni katika usimamizi mzuri wa mtu huyo hata kama mtu huyo hana au ana:-

(a) manufaa yoyote ya kisheria au vinginevyo katika hiyo mali; au

(b) haki yoyote, uwezo au faida kuhusiana na mali.

(2) Bila ya kupunguza ujumla wa kifungu kidogo cha (1), mahakama inaweza kuzingatia:-

(a) hisa katika, dhamana ya ushirika au ukurugenzi wa kampuni yoyote yenye manufaa ikiwa kama ni moja kwa moja au kwa kupitia mwingine katika hiyo mali; na

(b) muamana wowote ambao unahusiana au una mafao katika hiyo mali; na

(c) familia yoyote, mambo ya ndani au uhusiano wa kibiashara kati ya watu wenye manufaa na mali au katika kampuni au muamana uliorejewa katika aya ya (a) au (b) na watu wowote wale**,**

(3) Pale ambapo madhumuni ya kutoa amri ya adhabu ya kifedha dhidi ya mtu, mahakama itachukulia mali kama mali ya mtu huyo kufuatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), inaweza kwa maombi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoa amri inayotangaza kwamba mali imepatikana ili kutekeleza amri.

(4) Pale ambapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali anatuma ombi kuhusiana na kifungu kidogo cha (3)-

(a) atatoa notisi ya maandishi ya ombi kwa mtu huyo na kwa mtu mwingine yeyote ambae ana sababu za kuamini anaweza kuwa na manufaa katika mali hiyo; na

(b) mtu yeyote aliyerejewa katika aya ya (a) anaweza kuwenda mahakamani na kutoa ushahidi wakati wa kusikilizwa ombi hilo.

**24.** Kiasi kilicholipwa kuhusiana na amri za nchi za nje za adhabu za kifedha zilizosajiliwa katika mahakama za Jamhuri ya Muungano chini ya Sheria ya Kusaidiana, kiasi chochote kitakacholipwa, ikiwa ni katika Jamhuri ya Muungano, au katika nchi ya nje pale ambapo amri ilitolewa au kwingineko, katika kutekeleza amri ya nje ya adhabu ya kifedha, itachukuliwa kuwa imelipwa kama malipizi ya deni lililotokana na sababu ya usajili wa amri ya nje ya adhabu ya kifedha katika mahakama hiyo.

## SEHEMU YA NNE
## UTWAAJI KUHUSIANA NA MAKOSA MAALUM

Utwaaji wa mali ilyozuiwa kuhusiana na makosa maalum.

**25. -** (1) Kwa mujibu wa kifungu cha 43(4), iwapo katika kumalizika kwa miezi sita kutoka siku ya hukumu amri ya kuzuia ilipotolewa kuhusiana na mali ya mtu aliyehukumiwa kwa kosa maalum bado muda wake haujamalizika, mali itatwaliwa na Jamhuri ya Muungano.

(2) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3), mali iliyotwaliwa na Jamhuri ya Muungano chini ya kifungu kidogo cha (1) itapewa Msajili wa Hazina.

(3) Pale mali isiyohamishika au mali nyingine ambayo umiliki wake unapitia usajili inatwaliwa na Jamhuri ya Muungano, Msajili wa Hazina atastahili kusajiliwa kama mmiliki wa mali na waziri atakuwa na uwezo wa kufanya au kuamuru kifanywe, chochote cha lazima au muafaka kufanya usajili wa msajili wa hazina kama mmiliki, ikijumuisha utekelezaji na mtu anayehamisha manufaa katika mali ya aina hiyo.

(4) Pale Ambapo mali imetwaliwa na Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa kifungu hiki:

(a) mali haitashughulikiwa kwa namna yoyote ile isipokuwa, mpaka kwa ruhusa ya mahakama iliyotoa amri ya kuzuia na kwa kufuatia maelekezo ya mahakama mali inaweza kumalizwa au kushughulikiwa vinginevyo na au kwa niaba ya msajili wa hazina mpaka kama kutakuwepo na rufaa

itakayoanzishwa kuhusiana na jambo hili litaamuliwa au muda wa kuanzisha rufaa umepita bila ya rufaa yoyote kuanzishwa; na

(b) iwapo, mwisho wa muda uliorejewa chini ya aya ya (a), hukumu haijatanguliwa, mali inaweza kutumiwa au kushughulkiwa vinginevyo kufuatia maelekezo ya Waziri au mtu aliyeagizwa na Waziri kwa madhumuni ya aya hii.

(5) Maelekezo yoyote kuhusiana na aya ya (b) ya kifungu kidogo cha (4) yanaweza kujumuisha maelekezo kwamba mali itumiwe kulingana na sheria iliyoelekeza katika maelekezo. .

Upatikanaji wa mali ambayo kifungu cha 25 kinatumika

**26. -** (1) Pale mali imetwaliwa na Jamhuri ya Muungano kwa mujibu kifungu cha 25, mtu yeyote anayedai kuwa na manufaa katika mali hiyo anaweza, kutokana na kifungu kidogo cha (2) na cha (4), kuomba mahakama iliyotoa amri ya kuzuia mali hiyo kutoa amri chni ya kifungu kidogo cha (6)au cha (7).

(2) Ombi lililorejewa chini ya kifungu kidogo cha (1) litafanywa kufuatia kifungu kidogo cha (3), kabla ya kuisha kwa muda wa miezi sita tangu siku ile mali ilivyotwaliwa na Jamhuri ya Muungano.

(3) Mahakama inaweza kumpa mtu ruhusa kufanya maombi baada ya kuisha kwa muda uliorejewa chini ya kifungu kidogo cha (2) iwapo itaridhika kwamba kuchelewa kufanya maombi haikuwa kwa sababu ya uzembe.

(4) Maombi ya amri chini ya kifungu kidogo cha (6) au cha (7) kuhusiana na manufaa katika mali hayatafanyika, ila kwa ruhusa ya mahakama, na itafanywa na mtu aliyetoa notisi ya mwenendo wakati wa kutuma maombi ya kutolewa suala la kusimamishwa.

(5) Mahakama inaweza kumpa mtu ruhusa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4) iwapo itaridhika kwamba kushindwa kuwa na mali nje ya amri ya kuzuia haikuwa ni kwa sababu ya uzembe kwa upande wake.

(6) Pale ambapo mtu anaomba amri kuhusiana na manufaa katika mali na mahakama imeridhika:-

(a) kwamba mtuma maombi hakuwa amehusika kwa namna yoyote ile kuhusiana na utendaji wa lile kosa maalum lililohusika;

(b) pale ambapo mtuma maombi anapata manufaa wakati wa au baada ya kutendwa kosa , kwamba alifanya hivyo kihalali na kwa thamani ya kutosha;

(c) kwamba mali ile ilipatikana katika mazingira ambayo hayaleti wasiwasi adili kwamba mali ile siyo safi,

mahakama inaweza kutoa amri ikitangaza aina, kiasi na thamani ya manufaa ya mtuma maombi na itaelekeza msajili wa hazina kuhamisha manufaa hayo kwenda kwa mtuma maombi kwa kiasi kinacholingana na thamani ya manufaa.

(7) Pale ambapo mtu anatuma maombi kuhusiana na manufaa katika mali na mahakama ikiridhika kwamba haitakuwa kinyume na manufaa kwa umma kuhamishwa kwenda kwa yule mtu na kwamba hakuna sababu ingine kwanini manufaa hayo yasihamishwe kwenda kwa yule mtu, mahakama yaweza:-

(a) kuamua aina, kiasi na thamani ya manufaa ; na

(b) kuamuru kwamba kifungu cha 25 kiache kutumika kuhusiana na manufaa iwapo malipo kwa manufaa yanafanywa kulingana na kifungu cha 29.

Matokeo ya kutangua hukumu

**27. -** (1) Pale ambapo hukumu kuhusiana na mali iliyotwaliwa na Jamhuri ya Muungano kulingana na kifungu cha 25 inatanguliwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali:–

(a) haraka iwezekanavyo baada ya kutanguliwa kwa hukumu hiyo atatoa notisi ya maandishi kwa mtu yeyote ambaye Mwanasheria Mkuu wa Serikali ana sababu za kuamini kwamba angeweza kuwa na manufaa katika mali mara tu kabla ya kutwaliwa; na

(b) iwapo itaamuriwa kufanya hivyo na mahakama, atatoa notisi ya maandishi au kuchapisha notisi katika Gazeti la Serikali juu ya kutanguliwa kwa hukumu kwa mtu maalum au kundi la watu katika muda utakaopangwa na mahakama.

(2) Notisi kufuatana na masharti ya kifungu kidogo cha (1) itajumuisha maelezo ya mtu anayedai manufaa katika mali anaweza kutuma maombi kulingana na kifungu kidogo cha (3) ya kuhamisha manufaa kwa mtu.

(3) Mtu yeyote ambaye anadai alikuwa na manufaa katika mali mara kabla haijatwaliwa na Jamhuri ya Muungano anaweza kutuma maombi kwa Waziri kwa maandishi kwa ajili ya kuhamishia manufaa kwake na atakapopokea maombi ya aina hiyo,Waziri atalazimika:-

(a) iwapo manufaa hayo ni kuhusiana na mali iliyopewa Jamhuri ya Muungano ataandaa uhamisho wa manufaa kwenda kwa mtu huyo**;**

(b) katika suala lingine lolote, ataandaa malipo kwa mtu ya kiasi sawa na thamani ya manufaa.

(4) Katika kuandaa uhamisho wa mali yoyote kulingana na aya ya (a) ya kifungu kidogo cha (3), Waziri atakuwa na uwezo wa kufanya au kuamuru kufanywa kitu chochote cha muhimu au muafaka kufanya uhamisho ikijumuisha utekelezaji wa hati rasmi yoyote.

Mtu mwenye manufaa katika mali iliyotwaliwa anaweza kununua tena manufaa

**28. -** (1) Pale ambapo mahakama inatoa amri kufuatia kifungu kidogo cha (6) cha kifungu cha 16 kuhusiana na manufaa katika mali, malipo kwenda kwa msajili wa hazina ya kiasi kilichotajwa katika amri kama thamani ya manufaa itafuta amri ya kutwaa kwa kiwango kile kile kinachohusiana na manufaa.

(2) Pale ambapo mahakama inatoa amri kufuatia kifungu kidogo cha (7) cha kifungu cha 26, na malipo kwenda kwa Msajili wa Hazina ya kiasi kilichotajwa katika amri kama thamani ya manufaa imefanywa, kifungu cha 25 kitaacha kutumika kuhusiana na manufaa hayo.

(3) Waziri ataandaa manufaa yaliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) na cha (2) kuhamishiwa kwenda kwa mtu aliyekuwa amepewa mara kabla ya mali kutwaliwa na Jamhuri ya Muungano na atakuwa na uwezo wa kufanya, au kuamuru kufanywa kitu muhimu au muafaka katika kutekeleza ikijumuishwa hati rasmi yoyote.

Kununua manufaa mengine katika mali iliyotwaliwa

**29. -** Pale mtu ni kwa, kufuatia Sehemu hii, ameamuriwa kuchukua uhamisho wa manufaa katika mali iliyotwaliwa na Jamhuri ya Muungano, anaweza, kwa kutoa notisi kwa mtu yoyote mwingine vinginevyo mwenye kuitaka mali hiyo mara kabla ya kutwaliwa, kununua manufaa hayo mengine kutoka kwa Msajili wa Hazina, isipokuwa kwamba watu waliopewa notisi, wanaweza katika muda wa siku ishirini na moja tangu kupokea notisi hiyo, kupeleka kwa Waziri pingamizi la maandishi la ununuzi wa manufaa hayo.

Kutwaliwa ambako mtu hawezi kupelekwa mahakamani

**30. -** (1) Pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali anashuku kwa sababu adilifu kwamba mtu yeyote amepata, ameshikilia au anahusika na mali haramu na haiwezekani:-

(a) mtu mwingine kumleta mtu huyo mahakamani kwa shtaka la kosa kubwa; au

(b) kwa amri ya kutwaa ya nje ya nchi yenye fedha au amri ya nje ya kutwaa kutolewa kuhusiana na mtu huyo anaweza kutuma maombi Mahakama Kuu itoe amri ya kutangaza mali kutwaliwa na Jamhuri ya Muungano.

(2) Mahakama Kuu inaweza kwa maombi kufuatia kifungu kidogo cha (1), ikiridhika kwamba mali husika ni mali haramu na kwamba katika kutenda haki, mali hiyo itatwaliwa na Jamhuri ya Muungano, itaamuru ipasavyo.

## SEHEMU YA TANO
## UDHIBITI WA MALI INAYOTAKIWA KUTAIFISHWA

Uwezo wa upekuzi na ukamataji mali haramu

**31. -** (1) Kufuatia kifungu kidogo cha (2) afisa polisi anaweza kumpekua mtu na kukamata mali yoyote ambayo ataamini kwa sababu adili kwamba ni mali haramu.

(2) Upekuzi au ukamataji uliorejewa katika kifungu kidogo cha (1) utafanywa-

(a) kwa kibali cha mhusika; au

(b) chini ya hati iliyotolewa chini ya kifungu cha 32; au

(c) katika hali ya hatari kufuatana na kifungu cha 34.

(3) Kufuatia kifungu kidogo cha (2), afisa polisi anaweza kuingia kwenye ardhi au katika jengo, akapekua mali haramu na kukamata mali yoyote itakayokutwa wakati wa utafutaji ambao afisa anaamini kwa sababu adili, kuwa ni mali haramu**.**

(4) Katika kufanya upekuzi kulingana na kifungu hiki, afisa polisi anaweza pia kufanya upekuzi kwenye mavazi yaliyovaliwa na mtu huyo na mali yoyote iliyo kwa wakati ule chini ya uangalizi wake wa wazi; isipokuwa kwamba hakuna kitu katika kifungu hiki kitachukuliwa kwamba kuruhusu afisa polisi kuendelea na upekuzi kwa njia ya uchunguzi katika sehemu za maungo ya mwili**.**

Kusimamishwa kwa akaunti . Sheria Na.15 ya 2007 kif.11

**31A.** Pale Inspekta Jenerali wa Polisi au Mkurugenzi wa Mashtaka ana shaka kwa sababu adili kwamba mtu yeyote amehusika katika utendaji wa kosa kubwa, kosa la kusababisha au pesa haramu anaweza kuamuru na kumwelekeza afisa polisi wa cheo cha *ASP* au cheo cha juu zaidi kusimamisha akaunti ya benki na kukamata hati yoyote toka kwenye benki hiyo au taasisi ya fedha kwa siku saba wakati ambao ruhusa ya mahakama ya kukamata inaendelea

**32.** Hati ya upekuzi kuhusiana na mali haramu

(1) Pale afisa polisi ana sababu adili za kuamini kwamba kuna mali haramu aina fulani, kwenye mavazi yake au chini ya uangalizi wake wa wazi, au kwenye ardhi au katika jengo lolote, anaweza kumwomba hakimu kutoa hati ya upekuzi kwa mali haramu.

(2) Katika maombi kufuatana na kifungu kidogo cha (1), afisa polisi atamtaarifu hakimu kwa kiapo akielezea sababu ambazo zinapelekea kuombwa hati na hakimu anaweza, kufuatia kifungu kidogo cha (4),kutoa hati kumruhusu afisa polisi:-

(a) katika suala la hati ya upekuzi kuhusiana na ardhi au jengo, kuingia kwenye ardhi au jengo;

(b) kupekua mali haramu; na

(c) kukamata mali iliyokutwa wakati wa upekuzi ambao afisa polisi kwa sababu adili anaamini kuwa ni mali haramu.

(3) Hati ya upekuzi inaweza kutolewa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) kuhusu mali haramu iwapo au la taarifa ilikwishatolewa mbele ya hakimu kuhusiana na kosa husika.

(4) Hakimu hatatoa hati kufuatana na kifungu hiki mpaka awe ameridhika kwamba:-

(a) kuna sababu adili za kutoa hati; na

(b) iwapo taarifa itakuwa haijatolewa mbele yake kuhusiana na kosa husika wakati wa kutuma maombi ya kupata hati:-

(i) mali ni mali haramu; na

(ii) taarifa itatolewa mbele yake kuhusiana na kosa husika katika muda wa saa arobaini na nane.

(5) Hati iliyotolewa kufuatana na kifungu hiki itaelezea:-

(a) madhumuni ya kutolewa kwa hati ikijumuisha asili ya kosa husika;

(b) aina ya mali iliyoamriwa kukamatwa;

(c) tarehe ambayo hati itaacha kutumika; na

(d) wakati ambao umeamriwa kuingia kwenye ardhi au jengo.

(6)Iwapo wakati wa upekuzi chini ya hati ya utafutaji iliyotolewa chini ya kifungu hiki kwa mali haramu kuhusiana na kosa fulani, afisa polisi anagundua:-

(a) mali ambayo anaamini kwa sababu adili kuwa ni mali haramu kuhusiana na kosa,hata kama siyo ya namna ilivyoelezewa katika hati; au

(b) mali haramu inayohusiana na kosa jingine kubwa;au

(c) chochote ambacho afisa polisi anaamini kwa sababu adili kitaweza kutoa ushahidi wa utendaji wa kosa, na afisa polisi anaamini, kwa sababu adili, kwamba ni lazima kukamata mali hiyo au kitu ili kuzuia ufichaji, upotevu au uharibifu, au matumizi yake katika utendaji au kurudiwa kwa kosa hilo au kosa lingine lolote,hati hiyo itachukuliwa kumruhusu afisa polisi kukamata mali hiyo au kitu.

(7) Afisa polisi anayetenda kufuatana na hati iliyotolewa chini ya kifungu hiki anaweza kuhitaji mtu kuvua mavazi yoyote aliyovaa ikiwa tu iwapo kuvuliwa mavazi hayo ni muhimu na adili kuwezesha kumpekuwa sawasawa wa mtu huyo.

(8) Mtu hatafanyiwa upekuzi kufuatia kifungu hiki bali kwa kufanywa na mtu wa jinsia sawa na ukifanywa kwa kuzingatia staha.

Hati ya upekuzi inaweza kutolewa kwa simu

**33. -** (1) Iwapo kuna mazingira ya haraka na muhimu, afisa polisi akiona ni lazima kufanya hivyo anaweza kumwomba hakimu ampatie hati ya upekuzi kwa njia ya simu.

(2) Kabla ya kutuma maombi yaliyorejewa katika kifungu kidogo cha (1), afisa polisi ataandaa taarifa iliyorejewa katika kifungu cha 32(2).

(3) Baada ya maombi kufanywa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), hakimu anaweza, iwapo ataridhika baada ya kuzingatia taarifa iliyorejewa katika kifungu kidogo cha (2) au taarifa yoyote ile anayoweza kuipokea kuhusiana na sababu ambazo utoaji wa hati ya upekuzi uliombwa, kwamba kuna sababu adili za kutoa hati, atatoa hati na kuandika juu yake sababu za utolewaji wake.

(4) Pale hakimu ametoa hati kufuatia kifungu kidogo cha (3), atatoa taarifa kwa afisa polisi kuhusu masharti katika hati na tarehe ambayo na wakati ambao ilisainiwa na afisa polisi naye atajaza fomu ya hati kwa masharti yaliyotolewa na hakimu, ikijumuisha jina la hakimu.

(5) Si zaidi ya siku inayofuatia siku ya utekelezaji wa hati au kumalizika kwa matumizi ya hati, ni mapema, afisa polisi atampa hakimu aliyeamuru fomu ya hati kujazwa na taarifa kuhusiana na hati, kwa kutoa kiapo iliyoapishwa inavyotakiwa.

(6) Katika upokeaji wa nyaraka zilizorejewa katika kifungu kidogo cha (5), hakimu ataambatanisha hati aliyosaini na atazishughulikia kwa namna ambayo angezishughulikia kama maombi yangefanywa kufuatana na kifungu cha 32.

(7) Fomu ya hati iliyojazwa kikamilifu na afisa polisi kulingana na kifungu kidogo cha (4) itakuwa ni kibali cha upekuzi, uingiaji au ukamataji wowote.

Upekuzi katika hali ya hatari

**34. -** Afisa polisi anaweza kufanya upekuzi kwa mtu wa mali haramu au kuingia kwenye ardhi au katika jengo na kutafuta mali haramu na anaweza kukamata mali haramu atakayoipata wakati wa upekuzi iwapo:-

(a) anakiamini kwa sababu adili kwamba ni lazima kufanya hivyo ili kuzuia ufichwaji, upotevu au uharibifu wa mali haramu ; na

(b) upekuzi,uingiaji au ukamataji unafanywa katika mazingira ya dhati na ya haraka yanayohitaji na kuhalalisha upekuzi, uingiaji au ukamataji wa hapo hapo bila ya mamlaka ya amri ya mahakama au hati iliyotolewa chini ya sheria hii.

Wajibu kwa mali iliyokamatwa

**35. -** Pale mali imekamatwa chini ya Sehemu hii,Inspekta Jenerali wa Polisi au afisa mwingine aliyeamuriwa nae kwa maandishi, ataandaa mali kuwekwa na atahakikisha kwamba hatua zote adili zinachukuliwa ili kuitunza wakati imewekwa kwa jinsi hiyompaka itakapohitajiwa kwa madhumuni ya sheria hii au kuachwa kwa masharti ya sheria hii.

Kurudishwa mali iliyokamatwa

**36. -** (1) Iwapo mali ilikamatwa kufuatana na Sehemu hii na-

(a) inaonekana kwamba mali ilikamatwa vinginevyo kwa sababu zaidi ya kuweza kuwa ushahidi wa utendaji wa kosa;

(b) mwishoni wa kipindi cha saa arobaini na nane baada ya ukamatwaji, suala halijafikishwa mbele ya hakimu; au

(c) hakuna amri ya ukamataji itafanywa kuhusiana na mali katika muda wa siku kumi na nne baada ya hukumu ya mtu kuhusiana na mali; mtu yeyote ambae anadai ana manufaa katika mali anaweza kuiomba mahakama kutoa amri kwamba mali ile irudishwe kwake.

(2) Pale maombi yametumwa ili kusimamishwa au amri ya kutwaa kuhusiana na mali iliyokamatwa kufuatana na Sehemu hii inakataliwa, Inspekta Jenerali wa Polisi ataandaa mali hiyo irudishwe kwa mtu yule ambaye wakati wa kutwaliwa alikuwa anaimiliki haraka iwezekanavyo mara tu baada ya kukataliwa kwa maombi.

Upekuzi wa na ukamataji wa mali haramu kuhusiana na makosa yaliyotendeka nje ya nchi

**37. -** (1) Pale afisa polisi anaruhusiwa chini ya Sheria ya Kusaidiana kumwomba hakimu kupatiwa hati ya upekuzi chini ya sheria hii kuhusiana na mali haramu kuhusu kosa maalum la nje, masharti ya Sehemu hii yatatumika sawa sawa na ambavyo yangetumika kuhusiana na maombi ya hati ya upekuzi.

(2) Iwapo, wakati wa kutafuta mali haramu kuhusiana na kosa maalum la nje ya nchi, atatoa:-

(a) mali yoyote ambayo anaamini kwa sababu adili kuwa ni mali haramu kuhusiana na kosa maalum la nje ya nchi hata kama sio la namna ilivyoelezwa katika hati;

(b) mali yoyote ambayo anaamini kwa sababu adili kuwa ni mali chafu kuhusiana na kosa jingine maalum la nje ya nchi ambalo lilitolewa hati ya upekuzi ambayo bado inatumika;au

(c) jambo lolote ambalo anaamini, kwa sababu adili:-

(i) kuwa ni muhimu katika mwenendo wa jinai katika nchi ya nje kuhusiana na kosa maalum la nje; au

(ii) itasaidia kutoa ushahidi wa utendaji wa kosa la jinai, na anaamini, kwa sababu adili kwamba ni lazima mali au kitu kukamatwa ili kuzuia ufichwaji,upotevu

au uharibifu,au utumikaji,uendelevu au urudiwaji wa kosa au kosa lingine lolote,hati hiyo itachukuliwa kumruhusu afisa polisi kukamata mali au kitu hicho.

(3) Mtu yeyote ambaye anadai manufaa katika mali iliyokamatwa chini ya hati iliyotolewa kuhusiana na kosa maalum la nje ya nchi anaweza kuiomba mahakama impatie amri ya kwamba mali irudishwe kwake.

(4) Kwa maombi chini ya kifungu kidogo cha (3), iwapo mahakama itaridhika kwamba:-

(a) mtu yule anstahili ile mali;na

(b) mali ile sio mali haramu kuhusiana na kosa maalum la nje ya nchi,

mahakama itamwamuru inspekta jenerali wa polisi kurudisha mali kwa mtu yule.

(5) Pale mali imekamatwa kuhusiana na kosa maalum la nje ya nchi na mwishoni au kipindi cha siku thelathini baada ya siku ambayo mali ilikamatwa-

(a) hakuna simamisho la nje au amri ya kutwaa ya nje kuhusiana na mali imesajiliwa kulingana na sheria ya kusaidiana; na

(b) amri ya zuio ya muda, haijatolewa kufutana na masharti ya sheria hii kuhusiana na kosa maalum la nje ya nchi, Inspekta Jenerali wa Polisi ataandaa mali kurudishwa kwa yule aliyekuwa anamiliki mali kabla ya kukamatwa haraka iwezekanavyo mara baada ya kumalizika kwa muda ule.

Amri za kizuizi

**38. -** (1) Pale mtu amehukumiwa kwa kosa kubwa au amehukumiwa au anakaribia kuhukumiwa kwa kosa kubwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kuiomba mahakama kupewa amri ya kizuizi chini ya Sehemu hii dhidi ya mali yote au baadhi,ya mtu huyo ikijumuisha mali iliyopatikana baada ya kutolewa kwa amri ya kizuizi na mali ya mtu mwingine ambaye si aliyetiwa hatiani.

(2) Kwa maombi chini ya kifungu kidogo cha (1), mahakama inaweza, kwa mujibu wa kifungu cha 39:–

(a) kuamuru kwamba mali iliyotajwa katika maombi isiondolewe au kushughulikiwa vinginevyo na mtu yeyote isipokuwa katika namna na mazingira yaliyotajwa katika amri; au

(b) ikiridhika kwamba mazingira yanalazimu, kuelekeza kwamba mali au sehemu ya mali kama ilivyotajwa katika amri,ichukuliwe kutunzwa na kudhibitiwa na mdhamini aliyeteuliwa kwa madhumuni hayo na mahakama.

(3) Amri ya kizuizi dhidi ya mali ya mtu inaweza kutolewa kufuatia masharti ambayo mahakama itaona yanafaa na inaweza kuweka masharti ya kugharamia mali:-

(a) kwamba gharama adili ya maisha ikijumuisha gharama adili ya maisha ya wanaomtegemea na gharama adili za kibiashara;

(b) kwamba gharama adili za mtu huyo katika utetezi wa shtaka la jinai; na

(c) deni bayana aliloingia mtu huyo kwa nia njema likiwa ni deni ambalo aya ya (a) au (b) hazihusiki.

(4) Mahakama haitaweka masharti yoyote yaliyorejewa chini ya kifungu kidogo cha (3) mpaka ikiridhika kwamba mlalamikiwa hawezi kulipa gharama au deni husika kutoka kwenye mali ambayo haiko katika zuio.

(5) Pale mdhamini anatunza mali kufuatia kifungu hiki, anaweza kufanya chochote ambacho ni lazima kwa madhumuni ya kutunza mali, ikijumuisha:-

(a) kuwa mhusika katika shauri lolote la madai linaloathiri mali;

(b) kuhakikisha mali inawekewa bima; na

(c) iwapo mali kwa ujumla wake au kwa sehemu inahusika na biashara, kuajiri au kufuta ajira ya watu katika hiyo biashara.

Sababu za kutoa amri ya zuio

**39. -** (1) Pale ambapo kosa husika ni kosa maalum, mahakama kufuatia kifungu hiki itatoa amri ya zuio dhidi ya mali.

(2) Pale ambapo kosa husika ni kosa kubwa na sio kosa maalum, mahakama kwa mujibu wa kifungu hiki itatoa zuio dhidi ya mali isipokuwa kama mahakama imeridhika kwamba si kwa manufaa ya umma kutoa amri ya namna hiyo.

(3) Pale ambapo mlalamikiwa hajatiwa hatiani kwa kosa husika, mahakama haitatoa amri ya zuio mpaka:-

(a) maombi ya kupatiwa zuio yatathibitishwa na hati ya kiapo ya afisa polisi ikisema kwamba anaamini kwamba mlalamikiwa ametenda kosa hilo; na

(b) mahakama ikiridhika ikizingatia masuala yaliyomo kwenye hati ya kiapo kwamba kuna sababu adili ya kuamini hivyo.

(4) Pale ambapo maombi yamefanywa kusubiria kushitakiwa kwa mlalamikiwa kwa kosa husika, mahakama haitatoa amri ya kuzuiwa mpaka ikiridhika kwamba mlalamikiwa atashitakiwa kwa kosa au kosa linalohusiana katika muda wa saa arobaini na nane.

(5) Pale ambapo kosa husika ni kosa kubwa ambalo sio kosa maalum, mahakama haitatoa amri ya zuio dhidi ya mali ya mlalamikiwa mpaka:-

(a) maombi yanathibitishwa kwa hati ya kiapo ya afisa polisi ikisema anaamini kwamba:-

(i) mali ni mali haramu; au

(ii) mlalamikiwa alipata faida ya moja kwa moja au vinginevyo kutokana na utendaji wa kosa; na

(b) mahakama ikiridhika ikizingatia masuala yaliyoko katika hati ya kiapo,kwamba kuna sababu adili za kuamini hivyo.

(6) Pale ambapo amri ya zuio inatafutwa dhidi ya mtu mwingine mbali na mlalamikiwa, mahakama haitatoa amri ya zuio mpaka:-

(a) maombi yathibitishwe kwa hati ya kiapo ya afisa polisi ikisema kwamba anaamini kwamba:-

(i) mali ni mali haramu kuhusiana na kosa; au

(ii) mali inategemea udhibiti madhubuti wa mlalamikiwa aliyepata faida moja kwa moja , kutokana na utendaji wa kosa; na

(b) mahakama ikiridhika na kwa kuzingatia masuala yaliyomo katika hati ya kiapo, kwamba kuna sababu adili za kuamini imani hiyo.

(7) Katika kuamua kama kuna sababu adili za kuamini kwamba mali hiyo iko katika udhibiti madhubuti wa mlalamikiwa, mahakama inaweza ikizingatia masuala yaliyorejewa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 23.

(8) Amri ya zuio itatolewa kuhusiana na mali kama kuna ama hakuna hatari ya kutupiliwa mbali au kushughulikiwa vinginevyo mali hiyo kwa namna ambayo ingefanya ugumu katika utumikaji wa sheria hii.

(9) Mahakama inaweza kukataa kutoa amri ya zuio iwapo Jamhuri itashindwa kuipa mahakama uthibitisho ambao mahakama itaona unafaa kuhusiana na malipo ya gharama kwa uharibifu kutokana na kutolewa na kutumika kwa amri hiyo.

(10) Hati ya kiapo iliyotolewa na afisa polisi kwa madhumuni ya kifungu hiki itatoa sababu ambazo afisa zinamfanya ashikilie imani fuani..

Notisi ya maombi kwa amri ya zuio

**40. –** (1) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatoa notisi ya maandishi ya kuomba kupatiwa amri ya zuio dhidi ya mali kwa-

(a) mmiliki wa mali; na

(b) mtu mwingine yeyote amabae ana sababu za kuamini anaweza kuwa na manufaa na mali.

(2) Mahakama inaweza kutoa amri ya zuio bila kujali kwamba hakuna notisi ya maombi yamefanyika kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) iwapo itaridhika kwamba:-

(a) mazingira ya haraka na muhimu yanahitaji kutolewa kwa amri hiyo; au

(b) itakuwa kinyume na manufaa ya umma kutoa notisi ya maombi, lakini, kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3), amri ya zuio iliyotolewa kwa mujibu wa kifungu kidogo hiki itaacha kutumika mwisho wa kipindi hicho kisichozidi siku kumi na nne kama mahakama itakavyoelekeza.

(3) Mahakama inaweza, kwa maombi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kuisha kwa kipindi kilichorejewa chini ya kifungu kidogo cha (2) kuongeza kipindi cha matumizi kilichorejewa chini ya kifungu kidogo hicho iwapo mahakama inaridhika kwamba yapo mazingira yanayohalalisha ongezeko hilo na mmiliki wa mali au mtu mwingine yeyote anaweza kuwa na manufaa katika mali ataarifiwe kwa maandishi kuhusu maombi ya kifungu kidogo hiki.

(4) Mahakama inaweza kwa wakati wowote kabla ya uamuzi wa mwisho wa maombi ya kupatiwa amri ya zuio au kuongezwa kwa kipindi cha matumizi ya amri ya zuio,kumwelekeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuchapisha notisi ya maombi kwenda kwa mtu maalum au tabaka la watu kwa namna na katika kipindi kama ambavyo mahakama itaweka.

Watu wanaoweza kuwa mbele ya mahakama na kutoa ushahidi.

**41.** Pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa masharti ya kifungu cha 40, anatoa notisi ya maombi ya amri ya zuio au ya kuomba kuongezewa muda wa matumizi ya amri ya zuio, mtu yeyote anayedai kuwa na manufaa katika mali anaweza kuja mbele ya mahakama na kutoa ushahidi wakati wa kusikilizwa ombi.

Notisi ya amri za zuio

**42. -** (1) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), pale amri ya zuio imetolewa dhidi ya mali ya mtu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atampa mtu yule notisi ya maandishi ya amri.

(2) Pale mahakama imetoa amri ya zuio lakini imeridhika kuwa ni kwa manufaa ya umma kuchelewa kutoa notisi ya amri kwa mtu, mahakama inaweza kuamuru utoaji kwa mtu wa notisi ya amri ya zuio ucheleweshwe kwa kipindi kile kama kitakavyowekwa katika amri chini ya kifungu kidogo cha (1), na Mwanasheria Mkuu wa Serikali atampa mtu notisi ya amri ya zuio haraka iwezekanavyo baada ya mwisho wa kipindi kilichotolewa.

Mahakama inaweza kutoa amri zaidi ya hizo

**43. -** (1) Mahakama itakapotoa amri ya zuio, inaweza wakati inatoa amri hiyo au kwa wakati mwingine baadae kutoa amri nyingine ya ziada ambayo itaona ni muhimu, ikijumuisha:-

(a) amri inayobadilisha mali ambayo amri ya zuio inahusiana;

(b) amri inayobadilisha masharti yoyote ambayo amri ya zuio inahusu;

(c) amri ya uchunguzi kwa kiapo ya mtu (katika kifungu hiki ataitwa mjibu mashtaka amabae mali yake inategemea amri ya zuio, au mtu mwingine yeyote kuhusiana na mambo ya mjibu mashtaka, ikijumuisha asili na mahali mali ilipo ya mjibu mashtaka; au

(d) amri ya kutekeleza shughuli iliyofanywa na Jamhuri ya Muungano kuhusiana na malipo ya uharibifu au gharama inayotokana na kutolewa kwa amri ya zuio ; au

(e) pale mali iko katika utunzwaji au udhibiti wa mdhamini:-

(i) amri inayoelekeza namna ambavyo mdhamini anaweza kutekeleza uwezo wake au wajibu wake kuhusina na mali; au

(ii) amri inayoamua swali lolote kuhusiana na mali ikijumuisha swali lolote linalohusiana na madeni ya mjibu mashtaka;

(iii) amri inayoelekeza mjibu mashtaka kumpatia mdhamini katika kipindi kitakachowekwa maelezo kuhusu taarifa ya mali kama mahakama itakavyoona inafaa.

(2) Amri chini ya kifungu kidogo cha (1) inaweza kutolewa kwa maombi:–

(a) Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(b) kutoka kwa mjibu mashtaka;

(c) kutoka kwa mdhamini; au

(d) kwa ruhusa ya mahakama, mtu mwingine yeyote, na kila mtu mwingine mwenye manufaa katika suala atajulishwa na mtuma maombi kwa maandishi.

(3) Mtu yeyote mwenye manufaa katika mali ambayo inategemea amri ya zuio anaweza kuomba mahakama kubadili amri ya zuio ili kuondoa manufaa ya mtu kutoka kwenye amri na mahakama itakubali ombi hilo:-

(a) iwapo kosa husika sio kosa maalum na manufaa sio mali haramu; au

(b) pale kosa husika ni kosa maalum, iwapo itaridhika kwamba:-

(i) mwombaji hakuhusika kwa namna yoyote katika utendaji wa kosa; na

(ii) manufaa katika mali iliyopatikana kwa thamani ya kutosha,bila ya kujua, na katika mazingira ambayo hayaleti wasiwasi adili kwamba mali ilikuwa mali haramu.

(4) Ombi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3) inaweza kutolewa na mahakama iwapo mahakama inaridhika kwamba ni kwa manufaa ya umma kufanya hivyo ikizingatia mazingira ya kesi ikijumuisha:-

(a) matatizo ya kifedha au matokeo mengine ya manufaa yaliyobakia yakitegemea amri ya zuio;

(b) ule ukubwa wa kosa;na

(c) uwezekano kwamba manufaa inaweza kutegemea amri ya kutwaa au kifungu cha 25 au ikihitajiwa kuridhisha amri ya adhabu ya kifedha.

(5) Mtu yeyote ambaye ametiwa hatiani kwa au ameshtakiwa au anakaribia kushitakiwa kwa kosa maalum na ambae mali yake inahusika na amri ya zuio anaweza kuomba mahakama kuondolewa kwa mali yoyote kutoka kwenye amri ya zuio na mahakama itakubali ombi iwapo itaridhika kwamba:-

(a) mali hiyo haikutumiwa kuhusiana na utendaji wa kosa;

(b) manufaa katika mali ilipatikana kihalali.

(6) Pale mtu akichunguzwa mbele ya mahakama kufuatia amri chini ya kifungu kidogo cha (1), mtu yule hatasamehewa kutokujibu kwa sababu kwamba jibu linaweza kumpelekea au kumfanya awajibike kwa adhabu.

(7) Pale ambapo mtu siye ambaye mashtaka yamewekwa au yatawekwa ili yachunguzwe mahakamani kufuatia amri chini ya kifungu kidogo cha (1), maelezo au mafunuo yaliyo tolewa na mtu huyo katika kujibu swali lililowekwa wakati wa uchunguzi, na taarifa yoyote, waraka au kitu kilichopatikana kama matokeo ya moja kwa moja au vinginevyoya maelezo au mafunuo,hayatachukuliwa dhidi yake katika mwenendo wowote wa jinai isipokuwa mwenendo wa kutoa ushahidi wa uongo wakati wa uchunguzi.

(8) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (7), mwenendo katika maombi ya amri ya zuio, amri ya kutwaa,au amri ya adhabu ya kifedha haitachukuliwa kama ni mwenendo wa jinai.

(9) Pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaiomba mahakama kupatiwa amri kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), shahidi hatahitajiwa kujibu swali au kuwasilisha waraka iwapo mahakama imeridhika kwamba kujibu kwa swali au

kuwasilishwa kwa waraka kunaweza kuathiri uchunguzi wa, au kushitakiwa kwa mtu yeyote kwa, kosa.

Mdhamini kutekeleza **a**mri ya adhabu ya kifedha.

**44. -** (1) Pale mahakama imetoa amri ya adhabu ya kifedha dhidi ya mtu ambaye mali yake ya kifedha iko katika utunzwaji au chini ya usimamizi au udhibiti wa mdhamini, mahakama inaweza kumwelekeza mdhamini kuilipa Jamhuri ya Muungano kiasi kinacholingana na kiasi cha adhabu kutoka kwenye mali aliyoishikilia.

(2) Mahakama inaweza, kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), kuelekeza uuzwaji au vinginevyo kuondolewa mali yoyote inayotunzwa na mdhamini au chini ya udhibiti wake na kuamuru atekeleza hati rasmi yoyote iliyoko katika jina la mtu anayemiliki au mwenye manufaa au haki katika mali.

(3) Mdhamini hatatumia fedha kufuatia kifungu kidogo cha (1) au kushughulikia mali yoyote kufuatia kifungu kidogo cha (2) mpaka rufaa yoyote itakapokatwa kuhusiana na jambo lililokwisha amuliwa au kuhusu muda wa kukata rufaa yoyote umepita bila ya rufaa yoyote kukatwa.

Shtaka ya mali kufuatia amri ya zuio

**45. -** (1) Pale:-

(a) amri ya adhabu ya kifedha ikitolewa dhidi ya mtu akitegemea hukumu ya kosa; na

(b) amri ya zuio ni au imefanywa dhidi ya mali au mali ya mtu mwingine kuhusiana na amri chini ya kifungu cha 23(3) ni,au imefanywa ikitegemea hukumu ya kosa au kosa linalokaribiana au ikitegemea kushitakiwa kwake au pendekezo la kushitakiwa na kosa au kosa linalokaribiana, basi, katika kufanyika kwa amri ya mwisho kutaanzishwa kwa madhumuni ya kifungu hiki na bila uthibitisho wa ziada, shtaka juu ya mali ili kulinda malipo ya kiasi cha a dhabu yanayokwenda kwa Jamhuri ya Muungano.

(2) Pale shtaka limeanzishwa chini ya kifungu cha (1) juu ya mali ya mtu, shtaka litakoma kuhusiana na mali hiyo:-

(a) juu ya utanguzi wa hukumu iliyotegemea amri ya adhabu ya kifedha iliyofanywa;

(b) juu ya kuondolewa amri ya adhabu ya kifedha au amri ya zuio ya mahakama inayosikiliza rufaa dhidi ya utolewaji wa amri;

(c) juu ya mali kwenda kwa Jamhuri ya Muungano ya kiasi cha adhabu katika kutekeleza amri ya adhabu ya kifedha;

(d) juu ya mauzo ya mali kwa mnunuzi kwa nia njema kwa thamani, ambaye wakati wa ununuzi hakufahamu notisi ya shtaka, chochote ambacho kilitokea kwanza.

(3) Shtaka lililoanzishwa kwenye mali na kifungu kidogo cha (1):-

(a) litategemea vizuizi vyote katika mali ambavyo vilikuwepo kabla ya shtaka na ambavyo, bila ya kifungu kidogo hiki vingekuwa na kipaumbele juu ya shtaka;

(b) vitapewa kipaumbele juu ya vizuizi vingine vyovyote; na

(c) kufuatia kifungu kidogo cha (2), havitaathiriwa na badiliko lolote la umiliki wa mali.

(4) Pale shtaka limeanzishwa na kifungu kidogo cha (1) juu ya mali ya aina fulani na masharti ya sheria yoyote katika Jamhuri ya Muungano inaelezea usajili wa jina kwa,au mashtaka juu ya mali ya aina ile,mdhamini wa umma au Mwanasheria Mkuu wa Serikali,kama inavyoweza kuwa,anaweza kusababisha shtaka lilioanzishwa kusajiliwa chini ya masharti ya sheria hiyo na,iwapo shtaka litasajiliwa mtu

,atachukuliwa kuwa na notisi ya shtaka wakati wa ununuzi au kupata,kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2)(d).
Usajili wa amri za zuio

**46. -** Pale amri ya zuio imetolewa kuhusiana na mali isiyohamishika au mali yoyote au manufaa katika mali ambayo inatakiwa kusajiliwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atawasilisha maombi kwa msajili husika kwa ajili ya kuweka rekodi katika rejesta ya taarifa za amri.

Kuvunja amri za zuio
**47. -** (1) Kila mtu anayeondoa au vinginevyo anashughulikia mali ambayo kwa ufahamu wake imeegemea amri ya zuio atakuwa ametenda kosa na atatakiwa:-

(a) kama ni mtu binafsi , kulipa faini isiyozidi shiling laki tano au thamani ya mali, chochote ambacho ni kikubwa,au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na tano au faini na kifungo; au

(b) kama ni taasisi inayojitegemea, faini isiyozidi shilingi milioni tano au mara tatu ya thamani ya mali hiyo, chochote ambacho ni kikubwa.

(2) Jambo lolote lisiloruhusiwa kuhusiana na mali inayotegemea amri ya zuio litatupiliwa mbali na mahakama kwa ombi la Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Wajibu wa mdhamini
**48. -** (1) Iwapo, baada ya mdhamini kuelekezwa kulipa adhabu ya kifedha kutoka kwenye mali ya mtu, mdhamini atapewa notisi kwa maandishi ya mwenendo kufuatia sheria inayotumika kuhusiana na ufilisi dhidi ya mali ya mtu huyo, hatachukua hatua ya kuuza au kuondoa mali yoyote vinginevyo au kuilipa Jamhuri ya Muungano fedha zozote mpaka mwenendo wa ufilisi umemalizika.

(2) Pale mtu ambaye mali yake iko katika utunzwaji au udhibiti wa mdhamini anafilisika,mali hiyo itachukuliwa kuwa katika umiliki au udhibiti wa mdhamini kama, au kwa niaba ya mdhamini wa mali za mtu aliyefilisika.

Kulindwa kwa mdhamini kutoka uwajibikaji binafsi .
**49. -** (1) mdhamini hatawajibika kibinafsi kwa-

(a) upotevu au uharibifu unaotokana na utunzaji au udhibiti wa mali ambayo inatunzwa au kulindwa na mtu yeyote anayedai mali au manufaa katika mali mpaka mahakama ambapo dai limefanywa ina mawazo kwamba mdhamini ametenda kosa la uzembe kuhusiana na kuwa na ulinzi au udhibiti wa mali; au

(b) gharama ya mwenendo wa kesi ulioanzishwa kudai mali au manufaa katika mali

(2) Mdhamini hatawajibika binafsi kwa ushuru au kodi inayodaiwa chini ya sheria yoyote inayohusu mali iliyo katika utunzajia au udhibiti wake.

Ujira na gharama za mdhamini .
**50. -** (1) Mdhamini anastahili ujira na gharama kuhusiana na utendaji wa wajibu wake kuhusiana na mali iliyo katika ulinzi au udhibiti wake.

(2) Waziri atatayarisha kanuni zitakazochapishwa katika Gazeti la Serikali zinazoweka au zinazohusiana na ujira na gharama za mdhamini kuhusiana na utendaji wa wajibu wake chini ya sheria hii.

Mahakama inaweza kufuta amri za zuio
**51. -** (1) Mahakama inaweza, kwa maombi ya mtu dhidi ya amri ya zuio iliyokwisha kutolewa, kuruhusu amri ya zuio ifutwe iwapo mtu yule ataweka rehani

itakayoiridhisha mahakama kwa kulipa kiwango cha adhabu yoyote ya kifedha ambayo inaweza kuwekwa dhidi yake.

(2) Mtu ambaye amepeleka maombi kufuatia kifungu kidogo cha (1) atamjulisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali na, iwapo mali iko katika utunzaji au udhibiti wa mdhamini atamjulisha, mdhamini.

Amri ya zuio inapokoma kutumika

**52. -** (1) Amri ya zuio itakoma kutumika iwapo shtaka dhidi ya mtu kuhusiana na amri iliyotolewa inafutwa au iwapo mtu yule anaachiliwa.

(2) Pale mahakama imetoa amri ya utaifishaji, amri ya zuio itakoma kutumika mara baada ya amri ya utaifishaji kutekelezwa au vinginevyo kufutwa.

Amri ya zuio la muda kuhusiana na kosa la nje

**53. -** (1) Pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama alivyopewa mamlaka chini ya Sheria ya Kusaidiana kupatiwa utoaji wa mri ya zuio chini ya Sheria hii kuhusiana na kosa maalum la nje, masharti ya Sehemu hii kuhusiana na maombi ya amri ya zuio yatatumika kama ambavyo yatatumika kuhusiana na maombi ya amri ya zuio kuhusiana na kosa maalum la nje.

(2) Amri ya zuio, iliyotolewa kuhusiana na kosa malum la nje itakoma kutumika baada ya muda wa siku thelathini kuisha kuanzia siku amri ilipotolewa.

(3) Kwa maombi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya muda uliorejewa chini ya kifungu kidogo cha (2), mahakama inaweza kuongeza muda wa kutumika kwa amri ya zuio.

(4) Pale amri ya zuio haijasajiliwa Mahakama Kuu chini ya Sheria ya Kusaidiana, kabla ya kuisha kwa kipindi kilichorejewa katika kifungu kidogo cha (2) au cha (3) amri iliyorejewa katika kifungu kidogo cha (1) itakoma kutumika.

Amri za zuio ya nje zilizosajiliwa

**54. -** Pale amri ya zuio ya nje imesajiliwa Mahakama Kuu kwa mujibu wa Sheria ya Kusaidiana, masharti ya Sehemu hii yanayohusiana na amri ya zuio yatatumika kuhusiana na amri za au zuio zilizosajiliwa, kwa mujibu wa kifungu cha 55 na 56.

Mdhamini kudhibiti mali kuhusiana na amri yoyote iliyosajiliwa

**55. -** (1) Pale amri ya zuio ya nje imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano, mahakama inaweza kwa maombi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuelekeza kwamba mali au sehemu yoyote ya mali ichukuliwe kwa kutunzwa au udhibiti wa mdhamini aliyeteuliwa na mahakama.

(2) Mmiliki wa mali au mtu mwingine yeyote ambaye Mwanasheria Mkuu wa Serikali ana sababu za kuamini anaweza kuwa na manufaa katika mali atajulishwa kwa maandishi juu ya maombi yoyote kulingana na kifungu kidogo cha (7).

(3) Mahakama inaweza, kabla ya kutoa maelekezo kwa namna ya kifungu kidogo cha (1), atamwelekeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoa au kuchapisha notisi ya maombi kwenda kwa mtu maalum au tabaka la watu, kwa mujibu katika muda ambao mahakama inaona inafaa.

(4) Mtu yeyote anayedai kuwa na manufaa katika mali kutokana na maombi kufuatia kifungu kidogo cha (1) anaweza kwenda mahakamani na kutoa ushahidi wakati wa kusikiliza maombi hayo.

(5) Pale maelekezo yametolewa kufuatia kifungu kidogo cha (1), mahakama inaweza kwa wakati wowote kutoa moja au zaidi ya amri zifuatazo:-

(a) amri inayodhibiti namna mdhamini anavyoweza kutekeleza uwezo wake au wajibu wake;

(b) amri inayotoa maamuzi ya swali lolote kuhusiana na mali hiyo;au

(c) amri inayoelekeza mmiliki wa mali kumpatia mdhamini taarifa kuhusiana na mali kama mahakama itakavyoona inafaa.

(6) Mdhamini anaweza kufanya chochote anachoona ni adili na muhimu kwa madhumuni ya kutunza mali, ikijumuisha:–

(a) kuwa mhusika katika mwenendo wa kesi ya madai kuhusiana na utunzaji wa mali;

(b) kuhusika na kwamba mali imewekewa bima; na

(c) iwapo mali yote au sehemu inahusu biashara, kuiajiri au kusimamisha ajira ya watu katika biashara.

Shughuli ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**56.** Mahakama inaweza, kwa maombi ya mtu anayedai manufaa katika mali ambayo zinategemea amri ya zuio ya nje na ambayo iko katika utunzaji wa au chini ya udhibiti wa mdhamini, kutoa amri inayomhitaji Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoa au kuendesha shughuli kuhusiana na malipo ya uharibifu au gharama kuhusiana na amri ya zuio ya nje.

Kufutwa kwa amri za adhabu za kifedha za nje

**57. -** (1) Pale:-

(a) amri ya zuio ya nje imesajiliwa katika jamhuri ya muungano kuhusiana na mali ya mtu aliyehukumiwa kwa au aliyetuhumiwa kutenda ,kosa maalum la nje;

(b) amri ya adhabu ya kifedha dhidi ya mtu imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano kuhusiana na suala hili;na

(c) mali iliyo katika utunzaji, au chini ya udhibiti, wa mdhamini,

mahakama ambayo amri ya adhabu ya kifedha ya nje imesajiliwa anaweza kumwelekeza mdhamini kuilipa Jamhuri ya Muungano kiasi kinacholingana na kiasi cha adhabu kutoka kwenye mali.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) mahakama inaweza-

(a) kumwelekeza mdhamini kuuza au kuondoa mali hiyo iliyo chini ya udhibiti kama mahakama itakavyobainisha;na

(b) itampa mamlaka mdhamini kutekeleza hati yoyote au hati rasmi katika jina la mtu anayemiliki au ana manufaa au haki katika mali.

## SEHEMU YA SITA
## UWEZO WA KUKUSANYA TAARIFA
### Amri za Uwasilishaji

**58. -** (1) Pale ambapo mtu amehukumiwa, au inashukiwa kuwa ametenda kosa kubwa na afisa polisi ana sababu adili za kumtilia shaka mtu yoyote anamiliki au anadhibiti hati ya kufuatilia mali inayohusiana na kosa hilo anaweza kutuma maombi mahakamani kupata amri inayomwelekeza mtu yule,ikitegemea kufuatia kifungu kidogo cha (5), kuwasilisha kwa afisa polisi hati yoyote iliyoelezwa katika amri ambayo iko katika umiliki au udhibiti wa mtu yule.

(2) Maombi kufuatia kifungu kidogo cha (1) yatathibitishwa kwa hati ya kiapo inayoelezea sababu zinazopelekea shaka hiyo.

(3) Pale ambapo ombi kwa ajili ya kupatiwa amri kutokana na kifungu kidogo cha (1)afisa polisi amejumuisha kwenye hati ya kiapo iliyorejewa chini ya kifungu kidogo cha (2) taarifa kwamba ana sababu adili za kuamini kwamba mtu anayehusika alipata faida dhahiri au isiyo dhahiri, kutoka katika utendaji wa kosa na kwamba mali iliyotajwa katika hati ya kiapo inategemea udhibiti madhubuti wa mtu, mahakama

inaweza kuchukulia hati yoyote inayohusika kutambua,kuonyesha mahali,au kuelezea kiasi cha mali hiyo kama hati inayofuatilia mali kuhusiana na kosa kwa madhumuni ya kifungu hiki.

(4) Katika kutoa uamuzi kutokana na kifungu kidogo cha ( 3) ama kuchukulia hati kama hati inayofuatilia mali kuhusiana na kosa, mahakama inaweza kuzingatia masuala yaliyorejewa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 25.

(5) Amri ya kupatiwa hati haitatolewa hadi mahakama ijiridhishe kwamba kuna sababu adili ya kutoa amri.

(6) Pale hati inatolewa kwa afisa polisi, afisa polisi anaweza:-

(a) kukagua hati;
(b) kudondoa kutoka katika hati;
(c) kutoa nakala za hati; au
(d) kuishikilia hati iwapo, na kwa muda ambao kushikilia huko ni kwa lazima.

(7) Afisa polisi aliyerejewa katika kifungu kidogo cha (6), kwa ombi la mtu ambaye amri ile ameandikiwa:-

(a) atampa mtu yule nakala ya hati iliyothibitishwa na afisa polisi kwa maandishi kuwa ni nakala halisi ya hati hiyo; au
(b) atamruhusu mtu yule:-
   (i) kukagua hati;
   (ii) kudondoa kutoka kwenye hati; au
   (iii) kutoa nakala za hati.

(8) Mtu hatasamehewa kutowasilisha hati kwa sababu tu kwamba uwasilishaji wake:-

(a) unaweza kupelekea kumponza au kumfanya awajibike kwa adhabu; au
(b) itakuwa ni kuvunja makubaliano yoyote au upendeleo ambao sio wa kufichua kuwepo au yaliyomo katika hati.

(9) Uwasilishaji wa hati kufuatia kifungu hiki au taarifa yoyote, hati au kitu kilichopatikana kwa dhahiri au si kwa dhahiri katika uwasilishaji wa hati, hautakubaliwa kama ushahidi dhidi ya mtu yeyote, zaidi ya mtu ambaye shtaka limetolewa au litatolewa,katika mwenendo wa jinai isipokuwa mwenendo unaohusiana na:-

(a) ukiukwaji wa amri ya mahakama; au
(b) uwasilishaji wa hati inayojulikana kwa mtu yule kuwa ni ya uongo au inapotosha katika taarifa muhimu.

(10) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (9) mwenendo juu ya maombi ya amri ya zuio, amri ya kutwaa, au amri ya adhabu ya kifedha havitachukuliwa kuwa ni mwenendo wa jinai.

Kubadili amri ya uwasilishaji

**59. -** Pale mahakama inatoa amri ya uwasilishaji inayomhitaji mtu kuwasilisha hati kwa afisa polisi, mtu yule anaweza kuiomba mahakama ili kubadili amri na iwapo mahakama itaridhika kwamba ni muhimu kwa shughuli za kibiashara za mtu yule,inaweza kubadili amri ya uwasilishaji ili kumhitaji mtu yule kuwasilisha hati kwa afisa polisi kwa ukaguzi.

Kushindwa kutekeleza amri ya uwasilishaji

**60. -** (1) Pale mtu anahitajiwa kwa amri ya uwasilishaji kuwasilisha hati kwa afisa polisi au kufanya hati iwepo kwa afisa polisi kwa ukaguzi, mtu yule atakuwa ametenda kosa chini ya kifungu hiki iwapo:-

(a) atakua amevunja amri bila sababu adili; au

(b) katika maana ya jumla ya kutekeleza amri anawasilisha au kufanya kuwepo kwa hati ambayo itajulikana kwao kuwa ni ya uongo au inapotosha katika taarifa muhimu bila ya:–

(i) kuonyesha kwa afisa polisi aliyewasilishiwa hati, kwamba hati ni ya uongo au inapotosha; na

(ii) inatoa taarifa sahihi kwa afisa polisi iwapo mtu yule anayo au anaweza kuipata,taarifa sahihi.

(2) Kosa dhidi ya kifungu kidogo cha (1) kitaadhibiwa, akitiwa hatiani-

(a) iwapo mkosaji ni mtu asili, faini isyozidi shilingi milioni moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano, au faini na kifungo; au

(b) iwapo mkosaji ni kampuni, faini isiyozidi shilingi milioni tano.

Amri ya uwasilishaji kuhusiana na makosa ya nje .

**61. -** (1) Pale afisa polisi amepewa mamlaka kwa mujibu wa Sheria ya Kusaidiana kuiomba mahakama kupatiwa amri ya uwasilishaji chini ya Sheria hii kuhusiana na kosa maalum la nje ,anaweza kutuma maombi na kifungu cha 63 na 64 vitatumika ipasavyo kuhusiana na kosa maalum la nje.

(2) Pale afisa polisi anamiliki hati chini ya amri ya uwasilishaji iliyotolewa kuhusiana na kosa maalum la nje,anaweza kushikilia hati kwa kipindi cha mwezi mmoja akisubiri maelekezo ya maandishi kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu namna ambavyo hati hiyo itashughulikiwa,ambavyo inaweza kujumuisha maelekezo kwamba hati itumwe kwa mamlaka ya nchi hiyo ya nje iliyoomba kupatiwa amri ya uwasilishaji.

Uwezo wa upekuzi

**62. -** (1) Afisa polisi anaweza kuingia kwenye ardhi yoyote au katika jengo lolote na:-

(a) kufanya upekuzi katika ardhi au majengo kutafuta hati yoyote inayofuatilia mali kuhusiana na kosa kubwa;na

(b) kukamata hati yoyote iliyokutwa wakati wa upekuzi ambayo anaamini kwa sababu adili kuwa ni hati inayofuatilia mali kuhusiana na kosa Kubwa.

(2) kuingia kwa afisa polisi kutafanywa kwa ruhusa ya aliyeko kwenye ardhi au jengo au chini ya hati iliyotolewa chini ya kifungu cha 68.

Hati ya upekuzi na hati inayofuatilia mali

**63. -** (1) Pale mtu ametiwa hatiani kwa, au ametiliwa shaka kuwa ametenda kosa kubwa, na afisa polisi ana sababu adili za kuwa na mashaka kwamba kwenye ardhi au katika jengo kuna hati inayofuatilia mali kuhusiana na kosa hilo, afisa polisi huyo anaweza kuomba mahakama impatie hati ya upekuzi kuhusiana na ardhi au jengo na mahakama kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (5), itatoa hati ya upekuzi ikimruhusu afisa polisi, pamoja na msaada kama itakavyoona ni lazima:-

(a) kuingia kwenye ardhi au katika jengo lilioelekezwa chini ya hati kupekua kutafuta hati zilizoelezwa katika hati; na

(b) kukamata hati zozote zitakazokutwa wakati wa upekuzi ambazo afisa polisi anaaamini kwa sababu adili kuwa ni hati inayofuatilia mali.

(2) Maombi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) yatathibitishwa na hati ya kiapo ikitoa sababu zinazopelekea kuwepo na mashaka.

(3) Pale, katika ombi la kupatiwa hati kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), afisa polisi anajumuisha katika hati ya kiapo iliyorejewa chini ya kifungu kidogo cha (2) taarifa kwamba anazo sababu adili za kuamini kwamba mtu anayehusika alipata faida dhahiri au isiyo dhahiri kutoka katika utendaji wa kosa na kwamba mali

iliyotajwa katika hatii ya kiapo iko katika udhibiti madhubuti wa mtu huyo,mahakama inaweza kuchukulia hati yoyote inayohusika na kutambua ,kuonyesha na kupima kiasi kwamba mali hiyo kama hati inayofuatilia mali kuhusiana na kosa kwa madhumuni ya kifungu hiki.

(4) Katika kufanya uamuzi, kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3), kama kuichukulia hati kuwa ni hati inayofuatilia mali kuhusiana na kosa,mahakama inaweza kuzingatia masuala yaliyorejewa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 23.

(5) Hati ya upekuzi haitatolewa kufuatia kifungu hiki mpaka mahakama iridhike kwamba:-

(a) hati husika haitaweza kutambuliwa au kuelezewa kwa taarifa inayotosheleza kwa madhumuni ya kupata amri ya uwasilishaji;
(b) amri ya uwasilishaji imetolewa kuhusiana na hati na haijatekelezwa;
(c) amri ya uwasilishaji inaelekea kutotekelezeka;
(d) uchunguzi kwa madhumuni yale iliyotolewa hati ya upekuzi unaweza, kuathirika vibaya iwapo afisa polisi hataweza kupata hati bila ya notisi kwa mtu yeyote.
(e) kuna sababu adili za kutolewa hati.

(6) Hati ya upekuzi lazima ieleze:-

(a) madhumuni ya kutolewa kwake, pamoja na asili ya kosa kubwa aliloamini au limeaminika kutendeka;
(b) muda ambao kuingia kunaruhusiwa;
(c) maelezo ya aina ya hati zinazoruhusiwa kukamatwa; na
(d) siku, zisizokuwa zaidi ya siku thelathini baada ya kutolewa kwa hati, ambayo hati itakoma kutumika.

(7) Iwapo, wakati wa utafutaji wa hati fulani kuhusiana na kosa, afisa polisi anagundua:-

(a) hati ingine ambayo sio ya aina iliyoelezewa katika hati ya upekuzi lakini ambayo anaamini kwa sababu adili, kuwa ni hati inayofuatilia mali kuhusiana na kosa husika au hati inayofuatilia mali kuhusiana na kosa lingine kubwa; au
(b) chochote anachoamini kwa sababu adili kuwa kinafaa kuwa ushahidi katika utendaji wa kosa, anaweza, iwapo anaamini kwa sababu adili kwamba ni lazima kukamata hati au kitu ili kuzuia kufichwa kwake, upotevu au uharibifu, kukamata ile hati au kitu.

Uchunguzi wa akaunti ya benki . Sheria Na 15 ya 2007 Kif..13

**63A.** – (1) Bila ya kujali masharti ya sheria nyingine yoyote, Inspekta Jenerali wa Polisi anaweza,pale anapoona kwamba ushahidi wowote wa utendaji wa kosa kubwa, kosa muhimu au kusafirisha pesa haramu na mtu una uwezekano wa kukutwa katika akaunti ya benki ya mtu huyo,mke au mume au mtoto wa mtu yeyote anayeaminika kuwa ni mdhamini au wakala wa mtu huyo,na kwamba utaratibu wa kupata amri ya mahakama una uwezekano wa kuharibu utaratibu wa uchunguzi,kuruhusu kwa maandishi,afisa polisi yeyote wa au cheo cha Mrakibu Mwandamizi wa Polisi akiwa peke yake au na afisa mwingine yeyote, kuchunguza akaunti ya benki na ruhusa hiyo itatosheleza kuruhusu uwasilishaji wa akaunti ya benki kwa kuchunguzwa na afisa polisi huyo na afisa huyo anaweza kuchukua vivuli vya taarifa yoyote husika kutoka kwenye akaunti hiyo.

(2) Wakati wa uchunguzi, ikionekana ni lazima akaunti ya benki ishikiliwe kwa kipindi kisichopungua siku saba, afisa polisi aliyetajwa katika kifungu kidogo cha (1) atatakiwa kupata ruhusa ya mahakama ya kuendelea kushikilia hiyo akaunti ya benki .

(3) Mtu yeyote ambaye kutokana na kifungu kidogo cha (1) ameshindwa kuwasilisha akaunti ya benki anapohitajiwa kufanya hivyo au akimzuia afisa polisi kufanya uchunguzi wa akaunti ya benki au kuchukua nakala ya taarifa zozote husika kutoka katika akaunti ya benki anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kwa kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja au kwa vyote.

(4) Katika kifungu hiki "Akaunti ya Benki" inajumuisha leja, kitabu cha mahesabu, kitabu cha fedha taslimu na hati zozote ambazo hutumiwa katika shughuli za kawaida za kibenki na mtu anayefanya shughuli hizo, kama yake mwenyewe au kutumwa kama wakala na mtu mwingine, na kama ni maalum au vinginevyo, na kama ni shughuli za aina yoyote za kibenki iwapo mtu huyo mwenyewe ni benki au siyo kwa maana ya iliyomo katika Sheria za Benki na Taasisi za kibenki, ya mwaka 2005..

Kuwekwa chini ya ulinzi:-

**63B.** Kwa madhumuni ya kupata ushahidi kuhusiana na makosa makubwa,makosa muhimu, au kusafirisha pesa haramu,afisa polisi wa cheo cha Mraki Mwandamizi wa Polisi au cheo cha juu yake aliyeruhusiwa na Inspekta Jenerali wa Polisi au Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai anaweza kwa ruhusa ya mahakama:-

(a) kutumia data za kompyuta na huduma za mitandao;

(b) kuweka katika uchunguzi njia za kutunza taarifa ikijumuisha mashine za faksi,usafirishaji wa taarifa kwa elektroniki na njia za mawasiliano;

(c ) kurekodi tabia na vitendo au mazungumzo; na

(d ) kupata rekodi za binafsi za hati za viapo au Hati za taasisi za fedha na rekodi za kibiashara.

Ulinzi wa wachunguzi

**63C.** Hakuna adhabu itakayotolewa kwa mtu yeyote anyefanya uchunguzi wa kosa kubwa, makosa muhimu au kusafirisha pesa haramu amabaye kwa sababu ya kupata ushahidi anatekeleza kwa namna iliyoelezwa, vitendo ambavyo vingeweza kuchukuliwa kama misingi inayofanya kosa kubwa, makosa muhimu au kusafirisha pesa haramu au njama ya kutenda kosa la kupanga au kusafirisha pesa haramu.

Ruhusa ya mahakama

**63D.** Kwa madhumuni ya kupata ruhusa ya mahakama kufuatana na kifungu cha 63A na 63B, itatosheleza kwa Inspekta Jenerali wa Polisi au Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai kufanya maombi maalum ya kuthibitishwa kwa kiapo hata au pasipokuwa na kesi mahakamani.

Hati za upekuzi kuhusiana na makosa ya nje

**64. -** (1) Pale afisa polisi ameruhusiwa chini ya Sheria ya Kusaidiana, kupeleka ombi kupatiwa hati ya upekuzi chini ya Sheria hii kwa hati inayofuatilia mali kuhusiana na kosa maalum la nje, afisa polisi anaweza kuomba hati na kifungu cha 63 kitatumika sawa sawa kama kinavyotumika kuhusiana na ombi hilo.

(2) Pale afisa polisi anamiliki hati chini ya hati ya upekuzi kuhusiana na kosa maalum la nje, anaweza kuishikilia kwa kipindi kisichopungua siku thelathini akisubiri maelezo ya maandishi kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu namna ambavyo hati

itashughulikiwa, ambavyo inaweza kujumuisha maelekezo kwamba hati ipelekwe kwenye mamlaka ya nchi ya nje ambayo iliomba kupatiwa hati hiyo.

Amri za usimamizi

**65. -** (1) Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kutuma maombi kupatiwa amri ya usimamizi ikielekeza taasisi ya fedha kutoa taarifa za kibenki kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kuhusu shughuli za fedha zilizofanyika kupitia kwenye akaunti ya mtu fulani katika taasisi hiyo ya kifedha.

(2) Amri ya usimamizi itatumika kuhusiana na kumbukumbu za kifedha zilizofanywa katika kipindi kilichoelezwa katika amri.

(3) Mahakama haitatoa amri ya usimamizi mpaka iridhike kwamba kuna sababu adili za kutilia shaka kwamba mtu yule mwenye akaunti ambayo taarifa zake zinatafutwa-

(a) ametenda au anatiliwa shaka kutenda kosa maalum;

(b) alishiriki katika utendaji wa kosa au anatiliwa shaka ya kujihusisha na utendaji wa kosa maalum; au

(c) amefaidika dhahiri au kwa namna isiyo dhahiri kutokana na utendaji wa kosa maalum.

(4) Amri ya usimamizi itaelezea jina au majina ambayo akaunti inaaminika kushikwa na aina ya taarifa ambayo taasisi ya fedha inatakiwa kutoa.

(5)Taasisi yoyote ya fedha ambayo itavunja amri ya usimamizi au itatoa habari za uongo au zinazopotosha itakuwa inatenda kosa na atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni moja.

Kutofichuliwa kwa uwepo na utumikaji wa amri ya usimamizi

**66. -** (1) Taasisi ya fedha ambayo ni au imepatiwa amri ya usimamizi haitafichua ukweli huu kwa mtu yeyote isipokuwa wakili kwa madhumuni ya kupata ushauri wa kisheria au uwakilishwaji kuhusiana na amri.

(2) Inspekta Jenerali wa Polisi hatafichua kwa mtu yeyote zaidi ya afisa wa jeshi la polisi katika utendaji wa wajibu wake, uwepo wa amri ya usimamizi.

(3) Inspekta Jenerali wa Polisi hatatakiwa na mahakama yoyote kufichua uwepo wa amri ya usimamizi.

(4) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na kifungu hiki cha sheria anatenda kosa na atawajibika:-

(a) kama ni mtu binafsi, faini isiyozidi shilingi laki mbili au kifungo cha kipindi kisichozidi miaka kumi au vyote kwa pamoja;

(b) kama ni shirika/kampuni, faini isiyozidi shilingi laki mbili.

Amri za usimamizi kuhusiana na makosa ya nje

**67. -** (1) Pale afisa polisi ameruhusiwa kufuatia masharti ya Sheria ya Kusaidiana kutuma maombi mahakamani kupatiwa amri ya usimamizi chini ya Sheria hii kuhusiana na kosa maalum la nje, kifungu cha 66 kitatumika sawasawa kama ambavyo kingetumika kwa kosa maalum la nje.

(2) Pale Inspekta Jenerali wa Polisi anapatiwa taarifa ya amri ya usimamizi iliyotolewa kuhusiana na kosa maalum la nje atapeleka mara taarifa hiyo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Wajibu wa taasisi za fedha

**68.** [Kimefutwa,Sheria Na.15 ya 2007, Kif. 14]

Wajibu wa taasisi za fedha

**69.** [Kimefutwa,Sheria Na. 15 ya 2007 Kif.. 15]

**70.** [Kimefutwa,Sheria Na. 15 ya 2007 Kif.. 16] .

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA JUMLA

Kuingilia haki kumezuiliwa

**71. -** Mtu yeyote ambaye anatumia nguvu, vitisho, kuogofya, kuahidi, kutoa au kupokea kitu kwa manufaa yake kwa ajili ya:-

(a) kupata ushahidi wa uongo;

(b) kuingilia utolewaji wa ushahidi au upatikanaji wa ushahidi katika mwenendo; au

(c) kuingilia utaratibu wa kikazi wa hakimu, jaji, afisa mashtaka wa umma, wakili wa serikali au afisa yeyote ambaye anasimamia usalama wa sheria kuhusiana na kutendeka kwa makosa chini ya sheria hii,

anatenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kwa kifungo kisichopungua miaka mitano.

Kukatazwa kujihusisha na mali haramu

**72. -** (1) Hakuna mtu atajipatia, atamiliki au kwa namna nyingine yoyote atajihusisha na mali haramu.

(2)Mali haramu yoyote kuhusiana na kosa maalum la nje iliyopatikana, iliyomilikiwa au kushughulikiwa kinyume na kifungu hiki itawajibika kutwaliwa na Jamhuri ya Muungano kwa amri ya Mahakama Kuu kwa maombi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mwenendo wa wakurugenzi, maafisa, waajiriwa au mawakala.

**73. -** (1) Kwa madhumuni ya Sheria hii, pale ambapo ni lazima kutambua hali ya akili ya shirika au kampuni kuhusiana na kifungu kidogo cha (2) na kampuni itakuwa inatosheleza kuonyesha kwamba mkurugenzi, afisa, mwajiriwa au wakala wa kampuni hiyo au shirika na mwajiriwa au wakala ambaye mwenendo wake uliotumika wakati wa ajira yake, alikuwa na hali hiyo ya akili.

(2) Mwenendo wowote unaotumika katika na kwa niaba ya shirika au kampuni kwa:-

(a) mkurugenzi, afisa, mwajiriwa au wakala wa taasisi wakati wa ajira ; au

(b) mtu mwingine yeyote kwa maelekezo au kwa kibali, ama kwa uwazi au si kwa uwazi, wa mkurugenzi, mwajiriwa au wakala wa taasisi au kampuni, pale utoaji wa maelekezo au kibali uko katika uwezo wa mamlaka mkurugenzi, afisa, mwajiriwa au wakala, atachukuliwa kuajiriwa na taasisi, kampuni au shirika kwa madhumuni ya Sheria hii.

(3) Mwenendo wowote unaotumika na kwa niaba ya mtu ambaye si shirika au taasisi kwa:–

(a) mwajiriwa au wakala wa mtu katika eneo la mamlaka yake; au

(b) mtu yeyote mwingine kwa maelekezo au kwa kibali, pale utoaji wa maelekezo au kibali viko katika eneo la mamlaka ya mwajiriwa au wakala, atachukuliwa kuajiriwa na mtu aliyetajwa wa kwanza kwa madhumuni ya Sheria hii.

(4) Pale ambapo ni lazima kushuhudia hali ya akili ya mtu kuhusiana na mwenendo uliochukuliwa kufuatia kifungu kidogo cha (3) kuwa aliajiriwa na mtu huyo, itakuwa inatosheleza kuonyesha kwamba mwajiriwa au wakala wa mtu huyo akiwa ni mwajiriwa au wakala ambae mwenendo uliotumika uko katika eneo la mamlaka, alikuwa na hali hiyo ya akili.

(5) Rejeo lolote kwa kifungu hiki kwa hali ya akili ya mtu inajumuisha rejeo kwa ufahamu, nia, wazo, imani au madhumuni ya mtu huyo na sababu za mtu huyo kuwa ufahamu/nia, wazo, imani au madhumuni hayo.

Kujihusisha na mali iliyotwaliwa

**74. -** (1) Mtu anayejua kwamba amri ya kutwaa imetolewa kuhusiana na mali iliyosajiliwa, hatafanya jambo lolote mpaka amri ya kutwaa imefutwa, imeshughulikiwa au mali imeshughulikiwa vinginevyo kabla ya manufaa ya Jamhuri ya Muungano haijasajiliwa katika rejesta husika.

(2) Mtu akayekwenda kinyume au kushindwa au kukataa kutii masharti ya kifungu kidogo cha (1) anatenda kosa na atawajibika akitiwa hatiani-

(a) iwapo ni mtu binafsi kwa faini isiyozidi shilingi laki mbili au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au faini na kifungo;

(b) iwapo ni shirika au kampuni, kwa faini isiyozidi shilingi milioni tano.

Kigezo cha ushahidi

**75. -** Kufuatia kifungu cha 12, swali lolote la tendo litakaloamuliwa na mahakama kwa maombi chini ya sheria hii litaamuliwa kwa ulinganisho wa uhakikisho**.**

Rufaa

**76. -** (1) Mtu yeyote mwenye manufaa katika mali ambayo dhidi yake amri ya kutwaa ilitolewa anaweza kukata rufaa dhidi ya amri hiyo:–

(a) ikiwa ni mtu aliyetiwa hatiani ikitegemea amri ilivyotolewa, kwa namna sawa kama vile amri ilivyokuwa au ilikuwa sehemu ya hukumu iliyotolewa kwa mtu kuhusiana na kosa; au

(b) katika suala lingine lolote,kwa namna sawa kama vile mtu yule ametiwa hatiani kwa kosa ikitegemea amri ambayo imetolewa na amri ilikuwa au ilikuwa sehemu ya hukumu iliyotolewa kwa mtu kuhusiana na kosa.

(2) Mtu ambaye adhabu ya kifedha imetolewa dhidi yake anaweza kukata rufaa dhidi ya amri hiyo kwa namna sawa kama vile ilikuwa, au ilikuwa sehemu ya adhabu iliyotolewa kwa mtu kuhusiana na kosa ikitegemea amri iliyotolewa.

(3) Pale mahakama inatoa amri ya adhabu ya kifedha na inatoa amri hiyo chini ya kifungu cha 23(3) ikitangaza kwamba mali fulani ipo kutekeleza amri hiyo, mtu yeyote ambaye ana manufaa katika mali anaweza kukata rufaa dhidi ya amri chini ya kifungu cha 23(3) kwa namna sawa kama vile mtu yule ametiwa hatiani kwa kosa ikitegemea amri iliyotolewa na amri ilikuwa au ilikuwa sehemu ya adhabu iliyotolewa kwa mtu yule kuhusiana na kosa.

(4) Katika rufaa dhidi ya amri ya kutwaa, amri ya adhabu ya kifedha au amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 23(3), amri hiyo inaweza kuthibitishwa, kufutwa au kubadilishwa.

(5)Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kukata rufaa dhidi ya amri ya kutwaa, amri ya adhabu ya kifedha au amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 23(3) au dhidi ya kukataliwa na mahakama kutoa amri kama hiyo kwa namna sawa kama vile amri ilikuwa au ilikuwa sehemu ya adhabu iliyotolewa kuhusiana na kosa ikitegemea ile amri iliyotolewa**.**

(6) Hakuna kitu katika kifungu hiki kitachukuliwa kuathiri haki yoyote ya kukata rufaa ambayo mtu anaweza kupata zaidi ya kutoka katika kifungu hiki.

Gharama

**77.** Pale mtu analeta, au anakuwepo mahakamani wakati wa mwenendo wa kesi chini ya sheria hii ili-

(a) kuzuia amri ya kutwaa au amri ya zuio ili isitolewe dhidi ya mali; au

(b) kufanya mali yake iondolewe kutoka kwenye amri ya kutwaa au amri ya zuio, iwapo atafanikiwa ,na mahakama ikaridhika kwamba mtu yule hakuhusika kwa namna yoyote ile katika utendaji wa kosa kuhusiana na amri ya kutwaa au amri ya zuio iliyokuwa inatafutwa au kutolewa,basi mahakama inaweza kuamuru serikali kulipa gharma zote alizotoa mtu huyo katika kesi au sehemu fulani ya gharama hizi kama itakavyoamuliw a na mahakama.

Matumizi ya sheria zingine hazitaathirika

**78.** Hakuna kitu katika Sheria hii kitachukuliwa kama kupunguza au kuzuia:-

(a) utumikaji wa Sheria nyingine yoyote ya Jamhuri ya Muungano au ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayohusika na utwaaji wa mali iliyotwaliwa au utoaji wa adhabu za kifedha; au

(b) unafuu unaopata Serikali, zaidi ya Sheria hii, kwa kukazia haki na kulindwa kwa manufaa hayo.

Kanuni

**79.** Waziri anaweza kuandaa kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa madhumuni na masharti ya sheria hii, na kuagiza masuala ambayo:-

(a) yanahitajika au yana ruhusiwa chini ya Sheria hii kuagizwa;

(b) ni lazima au muafaka kuagizwa ili kutimiza malengo au utekelezaji bora wa sheria hii.